# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Hamsini na Sita – Tarehe 22 Juni, 2021

*(Bunge Lilianza saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Hamsini na Sita na kabla hatujaendelea nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wasaidizi wangu wote wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa David Kihenzile, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Najma kwa kazi nzuri ambayo wameifanya wiki nzima kutuendeshea mjadala wetu wa bajeti. *(Makofi)*

Sasa leo hapa ndio siku ya maamuzi ambayo kila Mbunge anapaswa kuwa humu ndani, kwa Mbunge ambaye Spika hana taarifa yake na hatapiga kura hapa leo hilo la kwake yeye. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali na tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela.

Na. 465

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri Katika Mji wa Laela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri ya Sumbawanga katika Mji wa Laela baada ya agizo la Serikali la kuhamisha Makao Makuu?
**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu la watu wa Kwela, Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni miongoni mwa Halmashauri 30 zilizohamia kwenye maeneo mapya ya utawala mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Halmashauri kutoa huduma bora kwa wananchi, Serikali imeweka mpango wa ujenzi wa jengo la utawala utakaogharimu shilingi bilioni 2.7

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imesaini mkataba wa ufundi na Chuo cha Sayansi Mbeya kwa ajili ya ujenzi utakaoanza tarehe 22 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukamilishaji wa jengo hilo, ahsante sana.

**SPIKA:** Nimekuona muuliza swali, Mheshimiwa Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunip nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kutupelea hiyo fedha shilingi bilioni moja. Nataka kujua sasa je, ni *commitment* gani ya Serikali kumalizia hizo fedha shilingi bilioni 1.7 ambazo zimebaki ili jengo hilo likamilike kwa kuwa wafanyakazi wa pale katika Halmashauri yangu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana?

Swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi ni *component* inaenda pamoja na ujenzi wa nyumba ya watumishi ikiwemo nyumba ya Mkurugenzi na Wakuu wa Idara. Nataka kujua je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha jambo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, majibu tafadhali; nyumba za Halmashauri kwa ajili ya watumishi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongezi zake kwa Serikali kwa kupeleka shilingi bilioni moja, lakini *commitment* ya Serikali tayari imetenga shilingi bilioni moja nyingine kwenye mwaka wa fedha 2021/2022 na shilingi bilioni moja tayari ipo Halmashauri ya Sumbawanga na kazi inaanza siku hii ya leo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwa mtiririko huu, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha tunakamilisha jengo la utawala katika Halmashauri ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, mpango wa ujenzi wa majengo ya utawala unaenda sambamba na mipango ya ujenzi wa nyumba ya watumishi kwa maana ya Mkurugenzi na Wakuu wa Idara. Kwa hiyo, safari ni hatua nimhakikishie wakati tunaendelea na ujenzi wa jengo la utawala pia

tunakwenda kuweka mipango ya kuanza ujenzi wa nyumba za Mkurugenzi na Wakuu wa Idara kwa awamu, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Tuanendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na. 466

**Kurasimisha Vitambulisho vya Wajasiriamali**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurasimisha vitambulisho vya wajasiriamali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tupo TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri - Dkt. Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2018, Serikali kwa kuwathamini na kuwajali wajasiriamali na watoa huduma wadogo ilianzisha utaratibu wa vitambulisho ili kuwawezesha kufanya biashara katika mazingira bora na tulivu zaidi. Vitambulisho hivi vilirasimishwa kutumiwa na wajasiriamali wenye mitaji yao na mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2021 vitambulisho vya wajasiriamali wadogo vimefanyiwa maboresho kadhaa ikiwemo kuwekwa picha na jina la mjasiriamali mdogo aliyepatiwa kitambulisho hicho pamoja na ukomo wa muda wa kutumia kitambulisho hicho. Muda wa matumizi ni mwaka

mmoja tangu tarehe ya kupatiwa kitambulisho badala ya mwaka wa kalenda kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha vitambulisho vya wajasiriamali wadogo kadri itakavyohitajika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu nimekuona.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapo wafanyabiashara ambao hawalipi ushuru, wamejitoa kwenye kodi na leseni kwa kisingizio cha kukosekana kanuni za vitambulisho vya mjasiriamali.

Ni nini kauli ya Serikali juu ya upotevu wa mapato unaosababishwa na wafanyabiashara hawa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa namna hali ilivyo huko site, vitambulisho hivi inaonekana kama ni hiyari, zoezi lake ni gumu na kwa wale wanaovikataa hakuna hatua yoyote ya kuwachukulia kikanuni.

Sasa ni lini Serikali itatoa kanuni hizo za vitambulisho vya mjasiriamali ili kuondoa mkanganyiko huo na kuweka bayana masharti na utaratibu wa vitambulisho hivyo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu maswali yako huwa makali. Majibu Mheshimiwa Festo Dugange, Naibu Waziri - TAMISEMI. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kimsingi vitambulisho hivi vilitolewa kwa nia njema ya kuhakikisha wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wanafanyabiashara kwa utulivu kwa kuwa na kitambulisho kinachowawezesha kutoa huduma zao za biashara bila kulipa gharama nyingine kama ilivyokuwa siku za kule nyuma.

Kwa hiyo, kanuni zimetolewa wazi kwamba kwanza ni mfanyabiashara mdogo, mwenye mzunguko wa biashara usiozidi shilingi milioni nne kwa mwaka lakini mfanyabiashara ambaye kimsingi anapatikana katika eneo husika linalofanyabiashara, lakini anaweza kufanya biashara sehemu nyingine; lakini kanuni nyingine ni kwamba kinatumika kwa miezi 12 tangu tarehe ile ya kukatwa kitambulisho kile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wafanyabiashara wadogo ambao hawalipii vitambulisho hivi, maana yake watakuwa tayari kulipa gharama zilizopo kisheria za kufanya biashara kwa maana ya ushuru mbalimbali na gharama zingine. Kwa hiyo, tunaendelea kuwaelimisha na walio wengi kwa kweli wanaona hii ni njia bora zaidi kwa sababu wanapata nafuu ya kulipa ushuru kila siku kwa kulipa kitambulisho kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, pili, vitambulisho hivi ni vya hiyari, lakini elimu inaendelea kutolewa ili walio wengi waweze kuona umuhimu wake na kuvitumia, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo sasa tunakuwa tumeshatoka TAMISEMI tunakwenda Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali. Mheshimiwa Latifa.

Na. 467

**Kuanzisha Mashindano ya Michezo wakati wa Sherehe za Muungano**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mashindano ya michezo mbalimbali kwa kila mwaka wakati wa sherehe za Muungano ili kudumisha hamasa za Muungano kwa vijana?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingiza, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, kuwa mashindano ya michezo kuelekea maadhimisho ya Muungano yalikuwa yanaleta hamasa kubwa kwa wananchi kila ifikapo Aprili kila mwaka. Kwa kutambua hilo, Serikali italifanyia kazi suala hili na Ofisi ya Makamu wa Rais itaratibu utekelezaji wake kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwani ni ukweli usiopingika kuwa michezo ina umuhimu mkubwa sana katika kudumisha Muungano wetu huu adimu na adhimu. Baada ya utekelezaji huo, Serikali itatoa taarifa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Latifa nimekuona.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mbali na majibu mazuri yaliyojibiwa na Mheshimiwa Waziri, lakini bado nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kama ni hivyo ndivyo, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba katika hayo mashindano ambayo mnaenda kuyaandaa yanaenda kuwaunganisha vijana wa kike na wa kiume moja moja kwa moja au asilimia 50 ya wanawake na asilimia 50 ya wanaume katika hayo mashindano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama hivyo ndivyo, Mheshimiwa Waziri ni lini mashindano hayo yataanzishwa kwa sababu tayari tulishaona katika mpango kazi mmetuambia kwamba hayo mashindano yataanza. Nahitaji *commitment* ya Serikali, ni mwaka gani hayo mashindano yataanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jafo, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri, lakini nimpongeze dada yangu Latifa kwa sababu miongoni mwa vijana ambao wamewakilisha Tanzania mwaka huu katika mjadala wa siku ya Muungano, Latifa alikuwa mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo, suala zima la kuhakikisha wanawake na wanaume wanashiriki kwa uzuri zaidi, tutalifanyia kazi. Na bahati nzuri kama unavyofahamu Serikali ya Awamu ya Sita imejielekeza huko kuhakikisha mchanganyiko wa jinsia zote mbili zinashiriki vizuri. Wasiwasi wangu ni kwa wanaume tusijetukajikuta kwamba idadi ya wanaume ikawa ndogo kuliko idadi ya wanawake katika michezo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika upande wa commitment jambo hili kwa sababu suala zima la uratibu na Wizara ya

Michezo kule Zanzibar na Wizara ya Michezo hapa Bara tutalifanya, baadae tutatoa taarifa rasmi katika suala zima la mchakato wa michezo hiyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali ma Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, uliza swali lako Mheshimiwa.

Na. 468

**Kutumia Bonde la Ruvu kwa Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Bonde la Ruvu linatumika kwa kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na changamoto ya usalama wa chakula?

**SPIKA:** Ahsante sana. Naibu Waziri Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, majibu ya swali hilo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete Mbunge wa Jimbo la Chalinze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bonde la Ruvu ni moja kati ya mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambacho kinasaidia uhakika wa chakula na kukabiliana na changamoto ya usalama wa chakula. Serikali imeianisha takribani skimu 21 zenye eneo la ukubwa wa takribani hekta 85,075 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Ruvu katika Mikoa ya Morogoro na Pwani. Aidha, jumla ya hekta 1,284 zimeendelezwa kwa kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji na wakulima wanatumia eneo hilo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuendeleza ujenzi na ukarabati wa

miundombinu ya umwagiliaji katika skimu zote zilizopo katika Bonde la Ruvu kama zilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Umwagiliaji wa mwaka 2018. Aidha, utekelezaji wa mpango huo umeshaanza katika skimu za Tulo (*Morogoro DC),* Msoga (*Bagamoyo DC*), Kwala (*Kibaha DC*) na Bagamoyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani, nimekuona.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali, lakini ninataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri; sasa ni lini Serikali itakuja na mkakati ulio mzuri zaidi ukiangalia kwamba maji yanayopotea katika bonde lile ni mengi sana na ile tija ya kilimo haipatikani katika lile ambalo tunaita usalama wa chakula katika nchi yetu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ridhiwani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *utilization level* ya Ruvu na mito mingine mikubwa katika nchi yetu haijafikiwa kiwango ambacho tunakitarajia na tunacho-*expect,* lakini hatua tulizochukua sasa hivi katika mpango wa umwagiliaji wa mwaka 2018 ambao tumeuandaa kama Wizara na hivi karibini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo ambayo tumekaa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kubadilisha *model* za *financing* za umwagiliaji na sasa tunaelekea kwenye mfumo wa *EPC* ambayo tutafanya miradi mikubwa ya kielelezo kwa ajili ya kuchagua maeneo machache na kuweza kuyapa kipaumbele na moja ya eneo ni Mto Ruvu na Mto Ruvuma.

**SPIKA:** Nimekuona pale mwisho kabisa, uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naitwa Michael Constantine Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini.

Naomba niulize swali la nyongeza; kwa kuwa Kibaha Vijijini kuna *scheme* ambayo inaendelea kujengwa lakini hijaaza uzalishaji na tatizo kubwa ni mifugo kuingia na kufanya uharibifu.

Je, Serikali itatusaidiaje kuondoa tatizo hilo kuhamisha wafugaji wale kwenda kwenye eneo la ufugaji la *NARCO* ili wakulima wa eneo lile walime kwa uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hili ni jambo *specific* na ni jambo linahusu sehemu moja, nitamuomba baada ya hapa tukae tukutane ili tukae na wenzetu wa Wizara ya Mifugo ili tuweze kulijadili na kulitatua kw apamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa mwisho kabisa.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika maeneo ambayo ameyasema Waziri kwamba yatajengewa *scheme* za uhakika, sikumsikia akitaja eneo la Ruvu Tambarare ya Same na Mto Ruvu huwa unaharibu sana eneo hilo. Je, ni lini sasa Serikali itawajengea watu wale *scheme* ya uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ruvu Tambarare kule kwa Mheshimiwa Anne Kilango eeh?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Hapana.

**SPIKA:** Ni kwingine, *okay.* Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa unapaelewa zaidi Ruvu Tambarare ni wapi, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la mama yangu, Mama Shally kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sijataja maeneo ya Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro; ni moja ya maeneo ambayo ni *potential,* kwa hiyo nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge waweze kutuvumilia, tumeunza huu mchakato na wenzetu wa Wizara ya Fedha na baada ya bajeti tutakuwa tuna kikao cha pamoja kwa ajili ya kuchagua maeneo yote ambayo yatakuwa ni ya miradi ya kielelezo katika umwagiliaji. Kwa hiyo, kila ambapo kuna *potential* na upande wa Kaskazini ni eneo muhimu sana kwetu kwa ajili ya uzalishaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Profesa Ndakidemi niliona kama ulitaka ku... umevuka eeh? Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, bado tupo Kilimo.

Na.469

**Mpango wa Kukwamua Wakulima wa Zao la Chai**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali katika kukwamua zao la zhai ambalo ni miongoni mwa mazao ya kimkakati yenye changamoto nyingi nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, bado tupo kwako tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa zao la chai kutokana na mchango wake katika Pato la Taifa, ajira kwa wadau wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa zao na kipato kwa wakulima wa chai. Katika kuongeza uzalishaji na tija ya zao la chai, Serikali inaendelea kuwekeza katika utafiti na uzalishaji wa miche bora ya chai ambapo hadi kufikia Mei, 2021, Taasisi ya Utafiti ya *TRIT* imefanikiwa kuzalisha aina mpya nane za miche za zao la chai zinazohimili ukame, ukinzani na magonjwa, zenye tija nzuri ya uzalishaji na ubora wa vionjo vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi za *TARI* na *TRIT* kwa kushirikiana na Kampuni ya Mbolea ya Minjingu inaendelea na majaribio ya mbolea ya Minjingu kwenye mashamba ya chai. Hatua nyingine ni kutoa mafunzo ya vitendo kwa wakulima 2,000 wa chai kupitia mashamba darasa 97 katika Halmashauri za Wilaya za Njombe, Rungwe na Mufindi kwa lengo la kuongeza tija, ubora na ushindani wa chai ya Tanzania kwenye masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuhamasisha wakulima wa chai kutumia umwagiliaji katika na baadhi ya wakulima chini ya makampuni ya Uniliver na *DL* wameanza kufanya majaribio ya matumizi ya mifumo ya umwangiliaji kwenye kukuza chai. Vilevile kupitia Mradi wa *Agri-connect* Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa ajili ya kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao ya chai, kahawa na bustani katika Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe na Katavi ambapo barabara zilizojengwa hadi kufikia Mei, 2021 zina urefu wa jumla ya kilometa 87.

Aidha, Mamlaka ya Mbolea Tanzania *(TFRA)* inaendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika katika zao la chai kutumia mfumo wa uagizaji wa mbolea *bulk* ambapo mwezi Februari Chama cha Ushirika wa Mazao na Masoko Mkonge kilifanikiwa kuagiza tani 500 mbolea aina ya *NPK* kwa ajili ya zao la chai.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha mfumo wa masoko ya chai na ifikapo Desemba, 2021 tutakuwa na mnada wa chai nchini Tanzania kwa mara ya kwanza ambao utafanyika Jijini Dar es Salaam na kutoa fursa kwa wazalishaji wakubwa na wadogo kushiriki kwenye uuzaji wa chai ndani ya nchi badala ya kupeleka chai kwenye mnada wa Mombasa nchini Kenya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe nimekuona.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali juu ya mpango wa zao hili la chai. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa tatizo kubwa la wakulima wa chai sasa hivi nchini ni kutokulipwa kwa wakati na wawekezaji; na viongozi wetu wa Serikali wamekuja Mkoa wa Njombe akiwemo Waziri wetu Mkuu na alitoa maelekezo wakulima walipwe kwa wakati lakini mpaka sasa wakulima hawajalipwa hela yao ya chai. Je, ni kauli ipi ya matumaini ya Serikali juu ya wananchi kulipwa fedha zao za chai? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa wawekezaji wengi waliopo sasa hasa Mkoa wa Njombe wanaonekana kutokuwa na uwezo na wakulima wamehamasika kufufua mashamba yao mengi ya chai hivi sasa.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kutafuta wawekezaji wengine kwa ajili ya zao la chai Mkoani Njombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu ya wananchi wa Lupembe kuhusu chai. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Swalle kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwa niaba ya Serikali kwamba Wabunge wa maeneo ya Mufindi, Lupembe na Mkoa wa Njombe kwa ujumla wamekuwa wakifanya jitihada kubwa sana kufanya *follow-up* kuonesha *stability* ya zao la chai. Na nipitie Bunge lako hili na kuwahakikishia Wabunge kwamba kampuni zinazosuasua ni kampuni mbili; Uniliver nalipa vizuri na hana matatizo na wakulima wote wanaomhudumia. Tumebaki na changamoto na Kampuni ya *DL* na mwekezaji wa *Lupembe Tea Company Ltd.*

Kwa hiyo, kupitia Bunge lako nataka tu niwahakikishie Wabunge kwamba tumewa-*summon* hawa wawekezaji wawili na tutakutana nao katika Ofisi ya Wizara ya Kilimo, Mwenyezi Mungu akitujaalia kabla ya tarehe 30. Na kwa kuwa Wabunge mtakuwepo, tutawahusisha katika kikao hicho ili tuweze kufikia *solution. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwekezaji wa Kampuni ya Lupembe, hana *option either* ku-*implement* tulichokubaliana ama apishe menejimenti kwa sababu Chama cha Ushirika ni sehemu ya *shareholders* wa ile kampuni; kaongoza kwa muda mrefu hatujaona *performance,* tutaweka menejimenti ya muda ambayo itahusisha watu watakaotoka ndani ya Serikali na ushirika na yeye ili waweze kuendesha kile kiwanda kwa sababu kwa muda mrefu tumempa nafasi na ameshindwa kutimiza wajibu wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi nimekuona.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa fursa na naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na bughudha wanazopata wafanyabiashara na wakulima wa soya wa Mikoa ya Ruvuma na Mbeya kwa sababu wanazuiliwa kuuza na kununua wanavyotaka na tunajua zao hili limepata soko huko China sasa hivi. Serikali inatoa kauli gani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Profesa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *position* ya Wizara ya Kilimo na Serikali ipo *very clear* na nitumie Bunge lako Tukufu kusema zao la soya Mkoa wa Ruvuma na mikoa yote inayolima soya halimo kwenye stakabdhi ya ghala. Ninaomba Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wasibughudhi mnunuzi yeyote anayeenda kununua kwa mkulima zao hili. Tumelisema kwa mdomo na tumeandika, tunarudia tena, asibughudhiwe mnunuzi yeyote anayenunua zao la soya, *volume* ya soya aina *economic viability* kuingiza kwenye stakabadhi ya ghala, bado *volume* ni ndogo. Wizara ya Kilimo ndio ina-*mandate* ya kutangaza zao gani liingie kwenye stakabadhi ya ghala. Tumesema mwaka huu waliondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao lingine ni choroko na dengu yaliyopo katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa hayaingii katika mfumo wa ushirika kwanza, tutayaingiza wakati utakapofika na tutakapoona kwamba sasa ni muhimu kufanya namna hiyo. Tumetoa *guidance* kwenye *price* wanachotakiwa Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya ni kufuatilia *guided price* iliyotolewa na Wizara ya Kilimo *as indicated price* kwenye masoko na wasiwabughudhi wanunuzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. JUSTINE L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, aHsante kwa nafasi hii.

Kwanza nashukuru sana kwamba Waziri wa Kilimo ametembelea shamba la chai pale Kilolo Jumamosi wiki iliyopita na kujionea mwenyewe lile pori ambalo nimekuwa nikilisema hapa. Na kwa kuwa Benki ya Kilimo iko tayari na ina fedha tayari kwa ajili ya kukopesha mwekezaji yeyote, sasa je, ni lini ule mchakato wa kutafuta mwekezaji utaanza

tena bada ya kuwa ulisimama katika kipindi hiki cha mwaka karibu mmoja uliopita? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, wananchi wa Kilolo wanakusikiliza huko Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Waziri wa Kilimo Profesa Mkenda amekuwepo huko wiki iliyopita akiwa pamoja na Mkurugenzi wa *Tanzania Agricultural Development Bank.* Baada ya muda mrefu kuhangaika kutafuta mwekezaji, *position* ambayo tunayo kama Wizara ya Kilimo na ambayo tutaenda kuitekeleza ni kuanzisha *special purpose vehicle* ambayo *shareholding structure* itawahusisha wakulima wadogo na *Tanzania Agricultural Development Bank* kwa sababu wao ndio wanaleta mtaji na wao wataleta menejimenti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba ule mpango wa kuhangaika kutafuta mwekezaji wa nje tumeachana nao, tutatumia *our own resources* kufufua hilo shamba na tutaweka menejimenti ambayo ita-*run,* kwa sababu tumefanya majaribio kwenye Vyama vya Ushirika vya KAKU, Mbogwe na Chato tumefanikiwa.

Kwa hiyo, huu ndio utakuwa mwelekeo kwenye maeneo ambayo tutaweka mitaji, tutaanzisha *special purpose vehicle,* halafu tutaendelea kufanya biashara na ushirika utashindana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na tuna maswali matatu kwenye Wizara hii. Tuanze na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Vijiji vya Bukoba.

Na. 470

**Ujenzi wa Barabara ya Kyetema - Katoro**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** Aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Kyetema – Katoro – Kyaka utaanza na kukamilika kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kyaka 2 – Kanazi – Kyetema yenye urefu wa kilometa 60.7 amepatikana na anatarajiwa kusaini mkataba mwishoni mwa mwezi Juni, 2021. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamlika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jasson Rweikiza nakuona, swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini majibu haya vilevile yaliwahi kutolewa huko nyuma kwa swali hilihili ambalo limewahi kuulizwa, lakini tukaambiwa hela imepatikana ya

msanifu na msanifu huyo hakuonekana na barabara hiyo mpaka leo haijawahi kujengwa. Sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara inafahamu umuhimu wa barabara au inajibu tu ilimradi kujibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa vile Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka jana imeiweka barabara hii kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami na kwa ville hata Ilani iliyopita ya mwaka 2015 ilikuwa na barabara hii, je, naweza leo kupata *commitment* ya Serikali kwamba ni lini ujenzi huu wa barabara hii kwa kiwango cha lami unaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mbunge wa zamani wa Jimbo hili la Bukoba Vijijini alikuwa anaitwa Mheshimiwa Sebastian Kinyondo na alikataa kabisa Jimbo hili kuitwa Bukoba Vijijini kwa sababu alisema Jimbo hili ni la Vijiji vya Bukoba sio Bukoba Vijijini kwa sababu Vijiji vya Bukoba ni kama miji midogo. *(Kicheko)*

Naomba swali hilo la Vijiji vya Bukoba lijibiwe sasa na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu umuhimu wa barabara hii. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inatambua umuhimu wa barabara hii na ndio maana mwenyewe anafahamu kwamba ana vijiji karibu 29, vijiji 18 vipo katika barabara hii kwa hiyo ikijengwa ni wazi kwamba uhakika wa yeye kuendelea kuwa Mbunge wa Bukoba Vijijini utakuwa umetimizwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2020/2021 kuna fedha milioni 557 zilitengwa kwa ajili ya kuendelea kufanya maboresho ili barabara hii iendelee kupitika wakati wote.

Vilevile mwaka wa fedha 2021/2022 zimetengwa fedha zaidi ya milioni 217 kwa ajili ya kuendelea kufanya maboresho. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba Wizara inajua umuhimu wa barabara hii na ndio maana imekuwa ikitenga fedha kutoka mwaka hadi mwaka ili kuendelea kuiboresha ili wananchi wa Bukoba Vijijini waendelee kupata huduma hiyo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili; ametaka kujua *commitment* ya Wizara. Kwenye jibu la msingi nimesema barabara hii tayari kuna mhandisi mshauri ambaye atafanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Na barabara hii kuna wahandisi wawili ambao wamepatikana; Mhandisi *consultant* ambaye atafaya kazi ya kutoka Kyetema – Kanazi – Katoro – Kyaka yenye urefu wa kilometa 60.7 atafanya kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, mhandisi wa pili *Age Consultant* yeye atafanya kazi sehemu ya barabara ya Bukoba, Bosimbe na Maluku yenye urefu wa kilometa 19.

Kwa hiuyo, wahandisi hao wawili wakifanya kazi hii ikikamilika sasa tutaanza angalau kilometa chache kufanya kazi ya ujenzi wa lami katika eneo hili ili Mheshimiwa Mbunge Jasson Rweikiza aendelee kuwa na uhakika wa kuendelea kuwa Mbunge wa eneo hili, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Wizara hii ina maswali mengi, naomba tuendelee na Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum Njombe. Kwa niaba yake endelea Mheshimiwa nimekuona.

Na. 471

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Njombe – Mdandu – Iyayi - Mbeya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa barabara ya Njombe – Mdandu – Iyayi kuelekea Mbeya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika**,** kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Njombe (Ramadhani) – Mdandu – Iyayi yenye urefu wa kilometa 74 ilikamilika tangu mwaka 2015. Kwa sasa ujenzi unaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo jumla ya kilometa 14.11 kati ya kilometa 74 tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami ikiwemo sehemu ya Mji wa kihistoria ya Mdandu.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 kipande cha kilometa 1.5 kinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi milioni 929.288 na katika mwaka wa fedha 2021/2022 kipande kingine cha barabara chenye urefu wa kilometa 1.5 kinatarajiwa kuanza kujengwa na inakisiwa kugharimu shilingi milioni 929.288. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili tu ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kibena Stop Lupembe kutokea Madeke ambayo inaunganisha Mkoa wa Njombe na Morogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ni lini Serikali itajenga kwa haraka barabara ya Makete ambayo inapita Hifadhi ya Kituro kutokea Mbeya. Sababu barabara zote hizi zina umuhimu kwa Mkoa wetu wa Njombe na zitaongeza uchumi wa Mkoa wa Njombe kwenye masuala ya utalii, lakini vilevile kwenye masuala ya biashara, naomba nipate majibu ya maswali haya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana umeeleweka. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Msongwe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibena - Kona kwenda Madeke ambayo inakuja kutokezea Mlimba, Ifakara ni barabara ambayo kwenye bajeti hii imetengewa fedha na itaanza kujengwa katika bajeti tunayoanza. Hali kadhalika, barabara aliyoitaja ya Makete - Isyonje kwenda Mbeya pia imepangiwa bajeti na itatangazwa katika mwaka wa fedha ujao. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara zote barabara zote mbili alizozitaja zipo na zimepangiwa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa mwaka ujao wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini uliza swali lako.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Ni lini Serikali itakamilisha barabara ya *Iringa bypass* kwa kilometa 6.8 zilizobaki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu la Manispaa ya Iringa, *Iringa bypass.*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara uliyoitaja ya kilometa 6.9 ni barabara muhimu ambayo itatuondolea adha pale ambapo changamoto ikitokea kati ya Ruaha na Mjini pakikwama basi mji unakuwa umefunga. Na Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba tayari tumeshaanza na katika bajeti tunayoanza, barabara hii utaendelea; lengo ikiwa ni kukamilisha hizo kilometa zilizobaki kwa ajili ya kuondoa hizo changamoto, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu mazuri ya matumaini kwa watu wa Iringa. Barabara hii Mheshimiwa Jesca ilimshinda kabisa Peter Msigwa miaka yote aliyokaa hapa, kwa hiyo, ukiijenga hii bwana tutafuatana siku ya ufunguzi kuonesha kwamba Jesca amefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Seleman Jumanne Zedi.

Na. 472

**Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Mbambali – Bukene - Kahama**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, ujenzi wa barabara ya Tabora – Mbambali – Bukene – Itobo hadi Kahama umefikia hatua gani baada ya kutengewa fedha kwenye bajeti mwaka 2020/2021?

**SPIKA:** Bado tupo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu ya watu wa Bukene tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Tabora – Mbambali – Bukene – Itobo yenye urefu wa kilometa 114. Kazi hii ilitekelezwa na Mhandisi Mshauri *NIMETA Consult* ya Tanzania na ilikamilika Aprili, 2020 kwa gharama ya shilingi milioni 790.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 1,000 sawa na bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati Serikali inaendelea na maandalizi ya kuanzia ujenzi wa barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi nimekuona.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Umuhimu wa barabara hii umeongezeka baada ya ule mradi mkubwa wa bomba la mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga, umeamua kujenga ile kambi kubwa itakayoandaa mabomba yote yatakayofukiwa njia nzima pembeni ya barabara hii na kwa kuwa wasimamizi wa mradi huu wale *ECOP* wana *package* ya miundombinu ya kuboresha barabara; na kwa kuwa kuna kakipande kama kilometa 50 mpaka 60 kutoka Nzega - Itobo mpaka kwenye ile kambi ambako mabomba yatapita.

Je, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi haioni umuhimu wa kukaa na hawa wasimamizi wa mradi huu wa *ECOP* kwa sababu na wenyewe wana *package* ya miundombinu wakashirikiana ili kipande hiki cha kilometa 50 mpaka 60 cha Nzega - Itobo mpaka Sojo ambako ni kipande katika barabara hii hii, wakashirikiana na wakapunguza gharama upande wa Serikali na huu mradi ukatoa fedha zake ili kukamilisha barabara hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya mapendekezo hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Zedi, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Zedi kwa mchango huo na mimi nimhakikishie Wizara pamoja na hawa watu wa *ECOP* tutakaa nao kuona uwezekano wa kujenga hiki kipande cha kilometa 50 hadi 60 kutoka Itobo hadi Nzega ili kuweza kurahisisha utengenezaji wa hili bomba, kwa hiyo mimi binafsi nimhakikishie Mheshimiwa nitafika Jimboni kwake na tuweze kuangalia uwezekano huo, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; kwa kuwa viongozi wa Kitaifa waliahidi pale Makambako kutengeneza barabara kilometa mbili za lami pale mjini. Ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya viongozi wa Kitaifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Msongwe, lami ya pale Makambako Mjini.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema sisi kama Wizara na Serikali kazi yetu kwakweli ni kuhakikisha kwamba zile ahadi zote zilizoahidiwa na viongozi wa chama na hasa ngazi ya kitaifa zinatekelezwa, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako ahadi hizo zitatekelezwa kulingana na fedha zitakapoendelea kupatikana na hasa katika kipindi hiki cha miaka mitano ambacho ndicho tumekianza, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda wa Kigoma.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona nilitaka kuulizwa swali la nyongeza kwamba viporo vya barabara zinazounganisha mikoa ni pamoja na viporo vya barabara ya eneo la Malagalasi - Uvinza kilometa 51 na kiporo cha barabara inayotoka Tabora kuja Nguruka kilometa 40; nataka nijue Serikali ni lini ujenzi wa viporo hivi kukamilisha barabara inayounganisha Mkoa wa Kigoma na Tabora vitakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kuhusu suala hilo kuhusu viporo vya barabara Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara alizozitaja za Kaliua mpaka Chagu yenye kilometa kama 36 tayari mkandarasi yupo *site* na amepiga kambi Kijiji cha Usinge, kwa hiyo ujenzi unaanza, lakini katika barabara ambazo zimetangazwa mwezi huu ambazo zinafadhiliwa na Mfuko wa *OPEC* kutoka Malagalasi hadi Uvinza yenye kilometa 51.3 tayari barabara

hii imeshatangazwa kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi kwa kiwango la lami na hivyo Mheshimiwa Kilumbe na wananchi wa Kigoma baada ya muda si mrefu kuanzia Dodoma mpaka Kigoma itakuwa ni kwa lami tu bila kugusana na vumbi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tuendelee sasa kidogo Waheshimiwa na Maliasili na Utalii swali litaulizwa na Mheshimiwa *Sister* Cecilia. *(Kicheko)*

Na. 473

**Askari wa Hifadhi ya Msitu wa Marang kujichukulia Sheria Mkononi**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na baadhi ya askari wa *TANAPA* wanaolinda Hifadhi ya Msitu wa Marang inayopakana na Kata ya Buger Wilayani Karatu kujichukulia sheria mkononi na kuwaua wananchi wanaoingia kwenye hifadhi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Msitu wa Marang, hasa wafugaji wanapoingiza mifugo yao hifadhini na kukamatwa na askari wa hifadhi, hukataa kutii sheria bila shuruti na kupiga yowe maalum ijulikanayo kama HAYODAA ikiwa ni kiashiria cha hatari kwa kabila la Wairaki. Hivyo, wananchi wengi hujitokeza wakiwa na silaha za jadi zikiwemo fimbo, mishale, mapanga na mikuki ili kuwadhuru askari wa hifadhi na

kupinga ukamataji huo wa mifugo na kuchukua mifugo yao kwa kutumia nguvu.

Mheshimiwa Spika, yamefanyika matukio mengi ya askari kunyang'anywa silaha au mifugo iliyokamatwa hifadhini na wananchi ambapo husababisha kutokuelewana kati ya askari wa hifadhi na wananchi. Kati ya mwaka 2013 hadi 2020 jumla ya matukio saba yalitokea ambayo yalihusisha wananchi kuwashambulia askari wa hifadhi, kuwajeruhi na wengine kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau pamoja na wananchi wa maeneo hayo imeandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ambapo kwa sasa hati zinaandaliwa na baada ya uhakiki wananchi watakabidhiwa hati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia nimekuona.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza nisikitike kwa majibu yasiyoridhisha au niseme labda ya sitaki kutumia kauli kama ya uongo dhidi ya matukio haya ambayo yametolewa na Serikali, na imekuwa ni rahisi sana askari wa *TANAPA* kujichukulia sheria mkononi kuliko majeshi mengine yoyote, na hii inafanyika maeneo mbalimbali nchini.

Sasa swali langu la kwanza; tarehe 29 Desemba, 2020 wananchi saba waliingia hifadhilini ikisadikika wanakwenda kuchimba madini, wananchi wanne mpaka leo hawajulikani walipo na inasemekana wamechomwa moto hadi kufa na askari wa *TANAPA.*

Je, hao nao waliamua wenyewe kujichoma au askari wa *TANAPA* waliwachoma wananchi hao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tarehe 22 Oktoba, 2020 siku ya kupiga kura askari wa *TANAPA* waliwapiga risasi ng'ombe kumi wa mama mjane kwenye eneo hili mpaka leo mama huyu hajafidiwa wale ng'ombe sasa hawa ng'ombe nao walijipiga risasi wenyewe au askari wa *TANAPA* waliwapiga risasi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba maelezo yote niliyosema hapa ni kweli na akihitaji ushahidi tutautoa kama Serikali. Askari wetu ni wengi sana wanauawa na tumekuwa tukishambulia zaidi askari, lakini haya matukio yanatokea pande zote mbili kwamba askari wanakuwa kwenye sheria na kukabiliana na maeneo yao ya hifadhi kwa maana ya kuyalinda yale maeneo lakini inapotokea sasa wananchi kutotii sheria basi huu mtafaruku unatokea.

Mheshimiwas Spika, lakini kwenye hili analoliongelea kwamba waliingia na kuchomwa moto, mimi hilo siwezi kuliongelea hapa kwa sababu taarifa zake tulishawahi kuziongelea hapa kwamba ziko kwenye uchunguzi na *DNA* ilishapelekwa kwenye maeneo yetu ya uchunguzi na taarifa hizi ni za kiusalama zaidi, kwa hiyo, tamko la Serikal litakuja kutolewa baada ya uchunguzi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, na hili la risasi kwamba kuna ng'ombe walipigwa risasi pengine labda nimuombe Mheshimiwa atuletee uthibitisho kwamba wakati ng'ombe hawa wanauawa kama alikuwepo basi tuweze kulishughulikia, lakini vinginevyo ninaomba sana na nimuombe kama anavithibitisho vyovyote ambavyo askari

walienda kupiga hao ng'ombe atuletee na Serikali itachukua hatua, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, *TANAPA* walikuwa ni watu wazuri sana sijui *what has happened,* sijui ile *transformation* imewabadilisha walikuwa ni watu wazuri sana, sasa hivi malalamiko dhidi yao ni makubwa sana. *(Makofi)*

Kuna kazi fulani ninahisi mnatakiwa muifanye katika kuzungumza na askari wenu na *TANAPA* kwasababu maeneo kama haya yanayolalamika *Marang Forest* ilikuwa ipo nje ya *Manyara National Park,* kuna sehemu ni ya Wilaya ya Mbulu na kuna sehemu ya Wilaya ya Karatu na tukasaidi sisi tukaunda Kamati kufanya msitu ule uwe ni sehemu ya hifadhi, wananchi wakishatoa tu eneo kuwa ni sehemu ya hifadhi imeshakuwa ni masaka kwao na malalamiko kama hayo sio vizuri tuangalie kuna nini, shida gani ipo mahali.

Mheshimiwa Sendeka nilikuona alafu Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa mgogoro unaoendelea kati ya askari wetu wa uhifadhi na wananchi wanaozunguka katika msitu wa Marang unafanana kabisa na mgogoro unaoendelea hivi sasa kati ya wananchi wa vijiji vya Kimotorok kwa upande wa Simanjiro na Kijiji cha Kiushiuborko kwa upande wa Kiteto dhidi ya pori la *Mkungunero Game Reserve* askari wanaoishi *Mkungunero Game Reserve* na kwa kuwa mgogoro huu ni wa muda mrefu na ulifikia Serikali kukubali kurudisha eneo ambalo walipima kwa makosa kinyume na *GN* iliyotakiwa *Mkungunero Game Reserve* imebaki Kondoa sasa imevuka mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaamua sasa kuja kukaa na wananchi wa vijiji vinavyozunguka *Mkungunero Game Reserve* kumaliza mgogoro huu ili kuepusha maisha

wa watu na vitendo vinavyofanana na hivi ambavyo Waziri akihitaji, hata hapa ndani nitoe ushahidi wa vitendo vya kinyama walivyofanyiwa wananchi wa Kimotorok na wahifadhi, nitakupa kwenye simu yangu hii? Nitakupa nashukuru sana naomba swali langu lijibiwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu hawa sasa ni wa *TAWA* sio *TANAPA*, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi ambao aliutoa awali, lakini pia niweze kumjibu Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba tunapotaka kutatua tatizo lazima twende kwenye kiini cha tatizo. Wote tunajadili hapa na hakuna siri ni kweli yanatokea mapigano kati ya askari wa Maliasili pamoja na wananchi, lakini mapigano haya yanatokea ndani ya maeneo ya hifadhi.

Kwa hiyo kwanza Mheshimiwa Ole-Sendeka na Waheshimiwa Wabunge wote tusaidiane kuelimisha wananchi wetu kwanza tusiingie, na endapo wananchi wanaingia kwa bahati mbaya na akatendewa visivyo tutoe taarifa, tupate huo ushahidi, tuwawajibishe askari hawa ambao hawafanyi vizuri. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshawawajibisha askari kadhaa, nilitoa takwimu hapa, askari 61 tumewafukuza kazi kwa sababu ushahidi umeletwa. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge pale wananchi wetu ambapo wanafanyiwa ndivyo sivyo tuletewe ushahidi ili tuwashughulikie askari hawa, lakini na sisi tuna wajibu wa kuwashauri na kuwaelekeza wananchi wetu tusiingie kwenye maeneo haya yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili ameongelea suala la Mkungunero, tulifanya kikao mimi Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Mheshimiwa Olelekaita kuhusiana na Mkungunero kuhusiana na *dispute* ya mpaka wa Mkungunero na tukakubaliana tunapeleka wataalam kwenda kuhakiki mpaka huo kwa mujibu wa *coordinates* ambazo zimewekwa

kwenye *GN.* Niseme hapa kuna tatizo moja, katika maandishi katika maneno imesema ni Wilaya ya Kondoa lakini *coordinates* zimefika Wilaya ya Kiteto, sasa kitaalam zile *coordinates* zina *prevail,* kwa hiyo, wataalam waende wakatuoneshe *coordinates* hizi zinatakiwa kuvuka au zisivuke ili tutatue mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kondoa Vijijini yupo hapa leo? Mheshimiwa Ashatu upo.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI** Mhehimiwa Spika, nipo

**SPIKA:** Una neno hapo. Halafu atakuja Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI**: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Pori la Hifadhi la Akiba la Mkungunero ni tatizo kubwa ambalo limegharimu maisha wa wananchi wetu limegharimu maisha hata ya wanyama pori wenyewe.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kondoa wangependa kujua ni lini ripoti ya Mawaziri ambayo ilikuwa ni taarifa ni timu iliyoundwa na Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ikaenda timu ya Mawaziri nane kwenda kufanya kazi na kuzunguka kwenye mapori yote likiwepo Pori la Hifadhi ya Mkungunero. Sasa ni lini ripoti ile itatolewa kwa wananchi na mipaka ikajulikana ili matatizo ambayo wananchi wameyaishi kwa miaka 50 na zaidi yaweze kufika mwisho sasa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waziri wa Ardhi, majibu tafadhali Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili

na Utalii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili nilisaidia kuchangia na nikasema kwamba tumekubaliana tutapita kwenye maeneo haya yote ya migogoro ili kuhakiki kwa pamoja kwa kutumia idara inayohusika na upimaji wa ramani ambayo ipo chini ya Wizara yangu, kwenda kuhakiki maeneo yote haya yenye migogoro ili tuweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

Lakini nataka kumpa taarifa katika eneo hilo la Mkungunero timu ya Wizara yangu ipo huko wiki hii, kwa maombi ya Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, lengo ni kwenda kuhakiki mipaka ya Mkungunero kulinganisha na *GN* iliyoanzisha pori na ndicho kilichoombwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, kwamba yeye hapingi pori, lakini anataka kujua ana mashaka pori lina mipaka tofauti na ile ya *GN* kwa hiyo timu ya wataalam wa Wizara yangu na Wizara ya Maliasili wako Mkungunero hivi sasa kwenye pori hilo hilo wanafanya hiyo kazi ya uhakiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya matokeo ya ile timu ambayo iliagizwa na Serikali tulikuwa tumeshasema hapa kwamba tuliomba fedha mwaka huu na tumepewa kwenye bajeti hii, tunakwenda sasa kuwajulisha na Wakuu wa Mikoa wanajua.

Mheshimiwa Spika, lakini tunakwenda kutelekeza sasa uamuzi wa Baraza la Mawaziri yale maeneo ambayo wananchi wameachiwa tutakwenda kuwaonesha na yale maeneo ambayo yanaondoshwa ndani ya hifadhi tutakwenda kuwaonesha na yale maeneo ambayo yanakaa ndani ya hifadhi tutawaonesha na tutaweka mipaka inayoonekana.

Kwa hiyo shughuli hiyo hatujaifanya katika maeneo yale lakini mwaka huu Wizara ya Maliasili na ya kwangu tumepewa fedha tunakwenda kufanya kazi hiyo rasmi baada ya bajeti hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nilichotaka tu mjue Mkungunero maana yake ninyi mnashughulika ya Kiteto, kuna hiyo ya Kondoa ambayo hiyo nayo ni tatizo la miaka mingi kubwa sana, lakini tunashukuru kwa majibu haya ambayo umeyatoa, muende mkashughulike na hili jambo la Mkungunero lina miaka mingi sana, Mkungunero, Mkungunero miaka mingi sana tufike mahali liishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; swali langu linahusiana na suala la maaskari.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali juu ya kutuletea kituo katika Tarafa ya Milola, sababu ya msingi ni kwamba ndani ya tarafa ile kila usiku uchao, kila asubuhi kuna taarifa ambayo ninaipata juu ya wanyama hasa tembo kuja kuzunguka katika maeneo yale ambayo watu wanaishi na matokeo yake watu wanapoteza maisha yao na nilishasema watu wamepoteza maisha, mazao yanaharibika kila siku na tunaambiwa tulime, sasa hata kama watu watalima nini matokeo yake.

Naiomba Serikali inipe tamko au inihakikishie juu ya kuleta kituo katika eneo letu lile ili askari wale waweze kushughulika na wale wanyama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Salma ni askari anakuwa wa Halmashauri au unataka wa Wizara?

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Ikiwa wa Halmashauri sawa, ikiwa ni wa Wizara sawa, lengo ni kuhakikisha kwamba askari wanakuwepo na maisha ya wananchi yanakuwa salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya kama umeelewa Mheshimiwa Naibu Waziri basi majibu, sina hakika eneo hili liko ndani ya hifadhi au liko jirani au vipi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na utalii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niwape pole kwanza wananchi wa eneo lile kwa kuendelea kuvamiwa na tembo, lakini Serikali itapeleka askari pale ambao wataenda kulinda ili kupunguza kadhia hii ya wanyama wakali na waharibifu kama tembo.

**SPIKA**: Swali la mwisho kwa siku ya leo la Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Kalenga tafadhali.

Na. 474

**_Freelancer_ Kuzuiwa Kusajili Namba za Simu**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni uamuzi wa kutaka ifikapo tarehe 1 Mei, 2021 wasajili wa namba za simu za mkononi mitaani *(freelancers)* wawe katika maduka unaweza kufuta ajira zaidi ya 40,000 na kudhoofisha lengo lake la ajira milioni nane ifikapo mwaka 2025?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer* Andrew Mathew Kundo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tarehe 16 Februari, 2021 Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*

iliwaelekeza watoa huduma kutekeleza takwa la kikanuni la usajili wa laini za simu kibayometria kwa kuwatumia mawakala wanaokidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni ya 10 ya Kanuni za Usajili wa Laini za Simu ya 2020 *(The Electronic and Postal Communications (SIM Card Registration) Regulations, 2020 GN No. 112* ya 2020.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa *freelancers* kwenye sekta, kiuchumi na katika kulinda ajira zao, tarehe 14 Aprili, 2021 Serikali ilisitisha zuio kwa watoa huduma kutowatumia *freelancers* katika usajili wa laini za simu kibayometria, kwa kutoa taarifa kwa umma na kwa kuwaandikia watoa huduma barua ya kuondoa zuio hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na watoa huduma imetengeneza rasimu ya mwongozo wa kuwatambua na kuratibu kazi za *freelancers* ili kuondoa mapungufu yaliyojitokeza na kuweka bayana uhusiano kati ya watoa huduma na *freelancers,* ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kiswaga nimekuona.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri, pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa asilimia 90 mpaka 95 ya wateja wapya kwenye mitandao ya simu wanapatikana kutokana na mfumo huu wa *freelancer* na Kampuni yetu ya *TTCL* imekuwa ikisuasua katika kuongeza wigo wake.

Je, lini sasa *TTCL* au Wizara itaagiza *TTCL* waweze kutumia mfumo huu ili waweze kuongeza wigo wao?

Swali langu la pili ni kwamba mfumo huu wa *freelancer* siyo ajira kamili, *I mean* vijana wamekuwa wakilipwa kwa njia ya *commission* na haya makampuni kwa mfano yana vijana kama laki moja hivi ambao wako kwenye

mfumo huo. Sasa kutokana na kutokuwa na sheria inayotambua mfumo huu, hawa vijana wamekuwa wakitumia wakati mwingine *loophole* ya kuyashitaki haya makampuni kwamba wameajiriwa na hivyo kuleta hofu ya haya makampuni kuendelea kuajiri hawa vijana.

Je, Serikali italeta lini hapa sheria ili sasa itambue mfumo huu kwamba ni mfumo kamili ambao unasaidia kuajiri vijana wengi ambao hawana kazi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Andrew Mathew.

**NAIBU WAZIRI MAWASILIANO TEKNOLOJIA NA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga Gedion Mbunge wa Kalanga kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nimpongeze Mbunge wa Kalenga Mheshimiwa Kiswaga kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya Jimbo na wananchi wake wa Kalenga. Haya ni matakwa ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kupitia ukurasa wetu wa 96, 97, 98 na ukurasa wa 113 kuongeza wigo wa mawasiliano kufikia asilimia 94. Sasa kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tayari imeshatoa maelekezo kwa *TTCL* kuanza kutumia mfumo huu na mpaka sasa wana-*agrigator* watano na *freelancer* takribani 3000. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunasimamia hili ili waendelee kuongeza wigo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la kamisheni kati ya *freelancer* na watoa huduma ni suala ambalo Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba inaweka mfumo mzuri ambao utatumika katika kusimamia ili kuwepo na uwajibikaji kwa *freelancer* pamoja na watoa huduma ili kuhakikisha kwamba tunaondoa hili *gap* ambalo lilikuwa linasababisha na kutokana na uhalifu uliokuwa unatokea sababu ya *freelancer* kutumia hizi *national ID* kwa matakwa yao na si matakwa ambayo yamewekwa kisheria, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekamilika sasa tunatambua wageni walioko hapa Bungeni tunaanza na wageni wa kutoka *Water Mission Tanzania* ambao ni wageni wa Spika ni Ndugu David Gerlach - Mkurugenzi wa Shirika la *Water Mission Tanzania*. *Water Mission* Ndugu Gerlach na wenzake, hawapo? Nafikiri hawajafika hawa.

Tunaendelea pia wageni wa kutoka Benki ya Amana Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano Ndugu Dasu Mussa, karibu sana; pia yuko Mkuu waIdara ya Bidhaa na Sharia Ndugu Jamal Juma, ahsante karibu sana na Meneja Mkuu Tawi la Dodoma Athuman Julius, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua Benki ya Amana ni moja ya benki ambayo inatoa *terms* nzuri sana za masuala ya mikopo na kadhalika, kwa hiyo, ni vizuri kuwasiliana naoili kuona namna mnavyoweza kufaidika ninyi na wapaiga kura wenu na huduma zinazotolewa na benki ya Amana ni huduma za kipekee kabisa. *(Makofi)*

Wageni wengine 202 wa Mheshimiwa Spika, ni wanafunzi 200 na walimu wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma - UDOM wakiongozwa na Ndugu Evodius Laurent, wale wageni wa *UDOM* karibuni sana, sana, karibuni sana watoto wetu *UDOM* inatufanya tuwe *very proud* hapa Dodoma, mjitahidi sana katika masomo yenu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge *(LSP)* ni *UNDP Monitoring and Evaluation Specialist* Ndugu Paul Mlemya. Hawa *UNDP* na wenyewe siwaoni, nafikiri hawajaja.

Wageni 22 wa Waheshimiwa Wabunge wa Mheshimwa Ummy Mwalimu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI wakiongozwa na Ndugu Asifiwe Jonas, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Selemani Jafo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa kata za Kisarawe na viongozi wa chama, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kisarawe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Zuberi Kizwezwe, hawa ni watu wa Kisarawe, karibuni sana wana Kisarawe Mheshimiwa Waziri yupo hapa mmemuona anafanyakazi nzuri karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Jumaa Aweso - Waziri wa Maji ambao ni Viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu *Engineer* Anthony Sanga, karibuni sana, karibu sana Katibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambao ni Ndugu zake kutoka Pangani mkoani Tanga wakiongozwa na Ndugu Ramadhani Singano, karibuni popote pale mtakapokuwa. Leo tuna wageni wengi sana huenda wengine hawajapata nafasi humu ndani. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi - Naibu Waziri wa Maji ambao ni Mabalozi wa Usalama Barabarani kutoka Mbeya wakiongozwa na Ndugu Hatibu Luga, karibuni sana wana Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa *Engineer* Kundo Mathew - Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni wapiga kura wake na wajasiriamali kutoka Bariadi mkoani Simiyu wakiongozwa na Ndugu Nchama Ntunga, karibuni popote pale mtakapokuwa. *(Makofi)*

Wageni 57 wa Mheshimiwa Mary Masanja - Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi wa kozi ya utalii wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Lonyori Mollel, wale wa utalii karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Venant Protas ambao ni dada zake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Hilda,

Ndugu Salustia na Ndugu Lucky, karibu huenda wamekosa nafasi kwenye *gallery*. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ambaye ni mpiga kura wake kutoka Magu Ndugu Geofrey Nyoni, karibu Geofrey. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Jonas Mbunda ambao ni wanafunzi wa *UDOM* wanaotokea Mbinga mkoani Ruvuma wakiongozwa na Ndugu Omel Mwitumba, wale wa Mbinga wale kule, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya ambao ni wanafunzi na wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kutoka Dodoma wakiongozwa na Ndugu Christina Segu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 8 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni wanachuo kutoka Chuo cha *SAUT* Mwanza wakiongozwa na Ndugu Justina Benezeth karibuni. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya wanawake ya mkoa wa Songwe ligi daraja la kwanza wakiongozwa na Ndugu Joseph Onyango, Songwe. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni viongozi wa CCM kutoka mkoani Geita wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya Ndugu Muhoja Mapande. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni Meneja wa Shule ya *The Glory* ya Mafinga mkoani Iringa Ndugu Mathew Levi, wale pale. *(Makofi)*

Wanafunzi 37 na walimu watatu kutoka Taasisi ya Mafunzo ya Afrika Mashariki iliyopo Arusha ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanyakazi wanaongozwa na Ndugu Mary Gulamiwa, karibuni sana na wengine mpo

sijapata maelezo yenu nitayapata baadaye kidogo natumaini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo; moja, leo kuna semina ya *sports betting* saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa hii ni ya wote au ya watu gani? *Sports Betting* ni ya watu gani wamealikwa? mbona wameniletea leo sasa. Nitaangalia nini la kuwaambia na wengine baadaye.

Waheshimiwa kuhusu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge wa Viti Malaum mkoa wa Mara ambaye alipata ajali jana tarehe 21 Juni maeneo ya Manyoni, Singida taarifa nilizonazo mpaka sasa ni kwamba anaendelea vizuri na aliumia zaidi kwenye mkono wa kushoto, kwenye ubavu na kichwani kidogo, lakini anaendelea vizuri kabisa, yuko *stable* na muda si mrefu anaweza kujiunga nasi kuendelea na majukumu yetu, kwa hiyo msiwe na wasiwasi hata kidogo. *(Makofi)*

Ahsante sasa tunaweza tukaendelea nadhani.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Tuanze na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nimesimama kwa Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako.

Leo mapema baada ya swali ya Mheshimiwa Paresso kumejitokeza majibu kutoka kwa Naibu Waziri akidai kwamba hawana *evidence* kwa matukio ambayo yamekuwa yakiendelea ya wananchi kuuawa aidha kwenye hifadhi za misitu au mbuga zetu za wanyama.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matukio haya kwenye maeneo mbalimbali na hata kuna baadhi ya Wabunge humu wameshawahi kutoa maelezo binafsi na hata maswali mbalimbali yanaelezea ni jinsi gani ndugu zetu

wanapotea hata kwenye mbuga ya Serengeti ndugu zetu wengi sana wamepotea wa Wilaya ya Bunda, Tarime na hata Serengeti kwenyewe. Lakini hivi juzi tu katika Wilaya ya Kaliua Kata ya Usinge, Kijiji cha Kombe kuna nyumba ilichomwa na mle ndani inasemekana kulikuwa kuna mtoto mdogo naye akafia mle ndani na vyakula vingine vyote kwa sababu kwamba hiyo familia iko kwenye Hifadhi ya Isawima.

Mheshimiwa Spika, sasa bahati nzuri sana Bunge lako Tukufu huko nyuma lilishawahi kuunda Kamati Teule kipindi kile cha Operesheni TOKOMEZA ambapo ilienda ikadhuru na ikaua wananchi wengi sana kinyume kabisa na utu wa binadamu na haki za binadamu.

Sasa nimeomba mwongozo wako kwa sababu haya matukio yameendelea sana, ndugu zetu wengi sana wanapotea, wengine wanakutwa wameuawa, wengine hata hawarudi na ng'ombe wanapotea, na vitu kama vile. Sasa ningeomba Bunge lako Tukufu muongozo wangu ni kwanini Bunge lako Tukufu lisiunde Kamati Teule ili wapite maeneo yote ambayo wananchi hawa wamedhurika waweze kuwa na takwimu kabisa ni wananchi wangapi wamedhurika na nini kilitokea ili sasa Kamati yako Teule iweze kuja kuliambia Bunge na Taifa kwa ujumla kwa sababu inasemekana Serikali haina *evidence* kwamba kuna matukio, haina ushahidi kama matukio yanatokea ili sasa tufikie ukomo wa ndugu zetu kuuawa, kila mara tunalalamika Bungeni hamna hatua stahiki zinazochukuliwa. Mwongozo wangu ni huo.

**SPIKA:** Muongozo tunaotoa ni ushauri ule ambao tulitoa mwanzoni napokea kabisa *concern* za Wabunge kwa Waziri, Naibu Waziri kwa ujumla wake kwamba hebu kaongeeni na *TANAPA,* walikuwemo wenzenu wengine kabla yenu.

Nitatoa mfano wa Mheshimiwa Kagasheki walikuwa hapa na wenzake, hivi hivi inasemwa watu wanauawa wanabisha, inasemwa humu ndani watu wanauawa wanakanusha, tukaunda tume hapa tukaunda tume hapa

ya akina Mheshimiwa Lembeli ikaenda ikafanya utafiti ilileta mambo ya ajabu ya aibu kabisa.

Kwa hiyo nawaomba wenzangu msiingie kwenye mstari ule ule wa kujaribu kuwalinda watu ambao hawalindiki, mkazungumze na *TANAPA, TANAPA* siyo hii ya sasa hivi kuna nini *there is a problem somewhere* mkazungumze nao. *(Makofi)*

Wamegeuka kuwa sasa wao ndiyo majangili, wana-*repetation* ukiona unasemwasemwa vibaya kabisa kila wakati kutakuwa na shida fulani na hawa wananchi wakijua kwamba nikikutwa humu nauawa maana yake ni kwamba mwananchi yeyote aliyeingia huko kwa sababu yoyote ile sasa na yeye ni vita na askari na askari ni vita na wao, tunakuwa na nchi tunasema ina amani kumbe kuna *spots* fulani fulani zina vita ndani yake. Kwa hiyo tuwaangalie *TANAPA* wajue hawa ni watu ni raia wa kawaida.

Hawa mbona wameishi nao miaka yote huko nyuma vizuri kwa nini sasa hivi hali ni hii? *There is a problem somewhere* Mheshimiwa Waziri, nenda kakae na watu wako, wasikudanganye, wasikupe ripoti za juujuu. Tazama tu kuna shida mahali, maana yake wengi ni vijana wameajiriwa miaka hii ya karibuni huenda bado ni *trigger happy* wanafurahia tu kunanii, kwa hiyo, mkaliangalie Mheshimiwa Waziri likiendelea huko mbele kwa kweli hatutasita itabidi tuunde kitu fulani, na hivi vitu tukiviundaga havitokagi salama kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Ndiyo maana tunasema hebu kakaeni na hawa askari wenu mzungumze nao mmeona mara wapi, mara wapi, yote ni kuuwawa uwawa, kuchoma kufanyaje, ukatili katili ambao hauna sababu. *TANAPA* wanapaswa wajitazame warudi kwenye ubinadamu wa askari wa Tanzania, wafanye kazi kama polisi wanavyofanya kazi. *(Makofi)*

Kulikuwa na Mwongozo wa pili Mheshimiwa Zungu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru, *engine* ya ku-*accelerate* uchumi nchini ni viwanda na leo ajira nchini mwetu imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wanafunzi ambao wanamaliza vyuo vikuu, kulikuwa na mpango wa Serikali kuanzisha *industrial park* Bagamoyo, lakini *park* hii ikapata mgogoro wa kimikataba na sasa ikawa bado kuna sintofahamu katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wangu ninaomba kujua, kutokana na changamoto za ajira na Bandari ya Dar es Salaam kutokuweza kuingiza meli kubwa za *five generation* na sasa bandari ya Dar es Salaam ukipita katika fukwe za Dar es Saalam kuna meli zaidi ya ishirini hazina nafasi ya kuingia kwenye bandari kutokana na ufinyu wa nafasi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha mazungumzo tena ya Bandari ya Bagamoyo kuanzisha viwanda, kuleta ajira kwa watanzania na kukuza uchumi na kuwa na *gateway* ya bandari ambayo ni ya Bagamoyo? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana ni *point* ambayo Serikal imeisikia, ushauri wetu ni kwamba waendelee kulitazama jambo hili kwa ukaribu wa hali ya juu, nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa siku ya leo ni siku ya kipekee sana na tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya muda si mrefu atafuata Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Fedha, nashangaa hata hawajasogea hapa sijui wanasubi nini? Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Naibu Waziri mnapaswa muwe *site* sasa, karibu tunaanza mambo yetu.

Kanuni ya 126 inasema hivi kanuni yetu ya Bunge; Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Serikali utakapomalizika na tunaumaliza leo kwa mtoa hoja Mheshimiwa Waziri kuhitimisha hoja yake hapa na tutaifanyia uamuzi, Spika atalihoji Bunge litoe uamuzi wake wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya Ibara 90(2)(b) ya Katiba na uamuzi huo wa Bunge wa kupitisha au

kutokupitisha bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja, ndivyo kanuni inavyosema. *(Makofi)*

Na hiyo Ibara ya 90(2)(b) inasema; Mheshimiwa Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote isipokuwa tu kama Bunge limekataa kupitisha bajeti iliyopendekezwa na Serikali; yaani leo hapa mkikataa hii bajeti maana yake mmejivunja wenyewe, yaani hampo. *(Makofi)*

Ninyi wote mkiwa hampo na Serikali nayo haipo *automatically* kwa sababu Serikali inaundwa kwa kuanzia na Baraza la hili la Mawaziri ambalo lote lipo humu ndani, kwa hiyo kunakuwa hakuna kitu. Ni mwanzo wa vurugu kubwa ambayo haijapata kutokea katika nchi yetu.

Kwa hiyo zoezi hili ni muhimu sana tunaloenda kulifanya, nilipenda nisisitize hilo tuelewane kimsingi, maana mwingine anaweza akafikiri ni mchezo wa kuigiza tu, hapa sasa na ndiyo maana nimekuja kukaa mwenyewe leo nipo kabisa hapa. Hapa leo mtoto hatumwi dukani hapa. *(Makofi/ Kicheko)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2020 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadaliano yanaendelea, sasa nimwite moja kwa moja Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na uje hapa

mbele nitakupa dakika 15 halafu Mheshimiwa Waziri nitakupa saa moja ya kuhitimisha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na bajeti hii ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, aidha nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa mwongozo wake aliotupatia tukaweze kuwasilisha bajeti hii ya aina yake, bajeti ambayo imegusa wananchi na bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge wameiunga mkono kwa kiwango cha hali juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue fursa hii vilevile kuipongeza sana Kamati ya Bajeti ya Bunge lako Tukufu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Sillo na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Kigua na Wajumbe wote wa Kamati hii, pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao mizuri sana ambayo imesaidia sana katika kufanya tuweze kuwa na bajeti ambayo tutaikamilisha leo Mheshimiwa Waziri atawasilisha majumuisho yake ya ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kwenda moja kwa moja kwenye baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezichangia; hoja ya kwanza ambayo nilitaka kuizungumzia leo ni ufafanuzi wa hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wameizungumzia baadhi yao kuhusu miamala ya simu kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wapo Wabunge ambao walitaka kuona kwamba fedha hii ambayo inakusanywa kwa malengo mema kabisa, je, fedha hii ambayo inatozwa kodi kwa wananchi wote wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini mipango ya matumizi yake haijagusa miradi ya maendeleo ya kijamii kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa ufafanuzi huo naomba niseme neno moja kwa ufupi sana, Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muungano wa damu na ni muungano wa kindugu, si muungano wa vitu au maslahi hata waasisi wa Taifa hili kilichowashawishi na kuwafanya waweze kuunganisha nchi hizi mbili ni historia ya udugu wa damu baina ya pande hizi mbili tokea wakati kabla ya ukombozi wa nchi hii mpaka hivi sasa na haikuwa kwa sababu ya maslahi kwamba nani atapata nini na nani atafaidika na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wakati kila miaka ikielekea mbele na vizazi vinavyoendelea kuzaliwa na sisi wazee ndiyo tunamalizika malizika, basi utaona kwamba hii dhana inaanza kupotea uelewa wake na ndiyo maana wazee hawa waliamua kwa makusudi kabisa kuweka kwenye Katiba kuanzisha Mfuko wa Pamoja wa Fedha. Dhamira yake ni hiyo hiyo kuweza kubaini mapato na matumizi ya Muungano ili yaweze kutumika kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati mchakato huo unaendelea kama ambavyo tumeahidi wakati tunawasilisha bajeti ya Wizara siku chache zilizopita, hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuna baadhi ya mapato yake ambayo inaruhusiwa kukusanya yenyewe na hivi majuzi tu mliona Mheshimwia Waziri alivyozungumzia kwenye bajeti yake kuhusiana na mapato yanayohusu uhamiaji, kwa maana hiyo basi hatuoni tatizo lolote kwenda sambamba na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na hivyo tumewapa wataalam kazi ya kuchambua matumizi haya ili pale zitakapokusanywa, zile fedha ambao zitakusanywa kwa Zanzibar ziweze kupelekwa Zanzibar, zitumike kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kwamba tukifanya hivyo tutaweza kupanua ile dhana nzima ambayo tumekuja nayo ya kuhakikisha kwamba kila mtu analipa kodi na anafurahia hayo maendeleo ya kodi yake kwa sababu madhumuni ya kodi hii ni kugusa huduma za jamii, kodi hii ama tozo hizi zinagusa maisha ya watu watu moja kwa moja

katika sekta zote za kijamii muhimu ikiwemo afya, elimu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo limezungumzwa vile vile ni ile hoja ya kwamba taarifa ya ambazo zinatoka *BOT* kwenda masharika ya kimataifa hazina taarifa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, *BOT* ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa za kifedha zote ikiwemo sera ya fedha pamoja na taarifa zingine zote zinahusisha ama zinazingatia upekee wa Zanzibar kwa uchumi wa Zanzibar. Lakini hoja ya taarifa zinazotoka *World Bank* na yenyewe tunaona ni ya msingi. Hivyo basi kwa kuanzia tumeamua kwamba tutawashawishi Benki ya Dunia wafungue ofisi yao Zanzibar ili kuweka karibu na kuweza kutatua tatizo hili kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ambayo yamefanyika kurekebisha zinazoitwa changamoto za Muungano na tumeweza kwenda nazo vizuri tu, hata hili ambalo Wabunge wengi wamelalamikia kuhusiana na changamoto ya magari ambayo yanakuwa *registered* Zanzibar kutokufanya kazi upande huu naamini kabisa muda si mrefu, Mheshimiwa wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa wakati ambao ataona unafaa na kama utaratibu zitakazokua zimekamilika za Kiserikali hataleta mabadiliko ya Sheria ya Usalama Barabarani ambayo yataondoa moja kwa moja tatizo hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu. Kwa hiyo, kwa hayo makubwa tumemaliza hatuwezi kushindwa na hili dogo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ninalota kulizungumza ni changamoto ya upatikanaji wa mikopo nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi; mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha tunatumia rasilimali zetu vizuri ili tuweze kujitegemea, huo ndiyo mwelekeo wa msingi kabisa na ndiyo maana ukiangalia katika bajeti hii ni bajeti ambayo katika kipindi cha miaka kumi imeweza kuja na utegemezi mdogo

wa asilimia 8.1 kutoka kwa wahisani, lakini ni lazima tukope ili tuendelee kama ambavyo walioendelea wanaendelea kukopa. Lakini cha msingi mikopo hii ambayo tunakopa tunataka tuhakikishe kwamba inaendelea kulengwa katika miradi ya maendeleo ambayo inachochea uchumi wa nchi hii. Lakini tuhakikishe mikopo hii inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuepuka mazingira yote ya ubadhilifu na wizi wa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika kufanya hivyo Serikali yetu hii ya Awamu ya Sita imeendelea kuhakikisha kwamba inaimarisha mahusiano na Jumuiya ya Kimataifa na ninyi mashahidi kwa kipindi kifupi toka Mama Samia ameingia madarakani ameweza kuimarisha mahusiano ya kimataifa na tumeweza kupata mikopo yenye masharti nafuu ya zaidi ya dola 1500 kwa kipindi kifupi na mikopo hii ya masharti nafuu ni muhimu sana ili kwanza kuhakikisha tunalinda maadili na heshima na uhuru wetu, lakini vilevile tunapata mikopo haiwi mizigo kwa wananchi wa nchi hii yenye riba nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mikopo hiyo zaidi tunalenga kama ambavyo Kamati na Waheshimiwa Wabunge mmeshauri ni mikopo ile ya *concessional loans* na *semi concessional loans* ambao vilevile ina *element* ya *grant* ndani yake na masharti yake yanaridhisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja deni tunaendelea kukopa haliyakuwa tukiji-*proud* kwamba deni letu ni himilivu, kwa sababu ukiangalia takwimu mpaka Desemba, 2020 uwiano wa deni la mapato ya ndani ni asilimia 13.7 wakati ukomo ni asilimia 23; kwa hiyo tuko vizuri, ziko nchi majirani zetu wanakaribia kufika kwenye ukomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini maoni yenu kuhusiana na mchakato wa *sovereign credit rating* tumechukua na tunafanya kazi kama ambavyo tume ya Mheshimiwa Waziri imeelezwa na vilevile tutaendelea ku-*maintain* ukopaji wa ndani wa chini wa kiwango cha asilimia moja ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusiana na *projection* ya asilimia 5.6 ya ukuwaji wa uchumi kwamba ni ndogo sana. *Projection* hii imezingatia nadharia nzima ya hali ya ulimwengu wetu na mazingira yaliyonayo sasa hasa katika kipindi ambacho ulimwengu umekumbwa na janga la UVIKO 19. Hali hiyo imesababishwa hata uchumi wa dunia na wenyewe ukuaji wake *projection* yake iwe kwa asilimia sita kwa mwaka unaokuja, ingawa inatarajiwa vilevile mwaka 2022 kurudi katika kiwango cha asilimia 4.4 *almost* kiwango cha kawaida.

Mheshimiwa Spika, ukuwaji wa uchumi wa nchi zilizopo chini ya Jangwa la Sahara wenyewe unakadiriwa kuwa kwa asilimia 3.4. Kwa hiyo, sisi makadirio yetu asilimia 5.6 yamezingatia mazingira mazima ya hali ya uchumi wa dunia ingawa maoteo yetu kwa miaka mitano inayokuja kama ambavyo mpango unaeleza ni kufikia kiwango cha asilimia nane.

Mheshimiwa Spika, tumeweka mazingira mazuri na misingi mizuri katika bajeti hii ili malengo ya asilimia nane yaweze kufikiwa na mambo haya ambayo tumefanya miongoni mwao kwanza ni kuhamasisha matumizi ya malighafi zetu za ndani ili kuongeza mnyororo wa thamani, lakini pia kuimarisha miundombinu wezeshi hususani sekta ya usafirishaji kwa maana ya barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari halikadhali nishati na umemelakini kuhakikisha tunaimarisha uwekezaji na biashara wa sekta binafsi tunaamini kabisa mambo haya ndiyo msingi ya bajeti yetu tukiyasema vizuri ongezeko la ukuaji wa uchumi kwa asilimia nane kwa miaka mitano inayokuja tutaufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine la kuzingatia na lamsingi kabisa ni kwamba katika bajeti hii tumetenga asilimia 37 ya bajeti kwenye maendeleo ambayo yanachochea ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mengine ambayo nilitaka niyazungumze kwa haraka haraka kuna hoja kadhaa

ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza ikiwemo hoja hii *ETS,* lakini vilevile kulikuwa na hoja ya *gypsum* pamoja na hoja ongezeko la kodi kwa matrela haya.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kuongoza kikao kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri ambacho kilihusisha baadhi ya malalamiko mengi ambayo yalijitokeza kuhusiana na hii suala ya *ETS,* kwa hiyo, hatua ambayo tulichukua tuliona kuna umuhimu wa kuzikutanisha pande zote ili tuweze kujua, kusikiliza hoja za pande zote mbili na kutoa maamuzi sahihi. Katika kikao hicho ambacho mimi ndiye nilikuwa Mwenyekiti wake tulikubaliana yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza; tumekubaliana kwamba hoja ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na ukubwa wa gharama wa *ETS* ni sahihi, lakini tumekubaliana kwamba matumizi ya teknolojia hii ni muhimu sana katika kuhakikikisha kwamba tunadhibiti mapato ya Serikari. *(Makofi)*

Kwa hiyo maelekezo ambayo tumetoa ni kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kuweza kukutana na wadau hawa ili kufanya majadiliano ikiwemo pamoja na mambo mengine kuangalia uwezekano wa kuweza kushusha gharama hizi ambazo zinalalamikiwa ambao ni mzigo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati hilo linaendelea hali kadhalika tumewaelekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kujipanga ili siku zijazo zoezi hili waweze kulifanya wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kana kwamba hiyo haitoshi kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili tumekubaliana kwamba kuna haja ya kufanya upembuzi yakinifu unaojitegemea ili kubaini kwa undani kabisa masuala yote yanayohusu utekelezaji wa mradi huu na jambo hilo litasaidia kuweza kutupa mwongozo wa baadaye wa kuweza kutoa maamuzi sahihi ikiwemo wakati wa majadiliano ya kibiashara pamoja na wawekezaji wanaohusiana na

biashara ama hata ikifika mahali tumeweza wenyewe kufanya basi tuwe tunaweza kufanya tukiwa tuna taarifa ambazo za kitalaam na zimethibitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mambo ambayo mengine yamezungumzwa niseme tu kwa ufupi ni kwamba tumeyapokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na yale ambayo pengine kutokana na muda hatuwezi kuyaeleza najua Mheshimiwa Waziri ataeleza mambo mengi, lakini kwa sababu mambo ambayo yamezungumzwa ni mengi na hatutaweza kuyamaliza yote kwa leo.

Mheshimiwa Spika, tuhakikishie kwamba tumeyachukuwa na tutazingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge ikiwemo mambo haya mawili ambayo sikupata muda wa kuyazungumzia ya ile hoja ya *gypsum* pamoja na ongezeko la kodi ya ushuru wa forodha kwenye matrela, lakini tutayachukulia hatua kwa mujibu wa maelekezo na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha - *Engineer* Hamad Masauni tunakushukuru sana kwa mchango wako katika hoja hii.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana tunashukuru sana kwa kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa ruksa yenu nimkaribishe moja kwa moja mtoa hoja mwenyewe ili aje aihitimishe hoja yake Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba tafadhali karibu sana kama nilivyokuambia una saa moja karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze

kuhitimisha hoja niliyoitoa mnamo tarehe 10 Juni mwaka huu na kabla sijaanza kuhitimisha nianze kwanza kwa kutoa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa anayoijenga kwa wananchi wa Tanzania pamoja na Jumuiya za Kimataifa, pamoja na maelekezo yake ya mara kwa mara yanayotuwezesha tutekeleza majukumu yetu kikamilifu, hakika kazi zake anazozifanya zinafanya kazi yetu pia iwe nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson - Naibu Spika pamoja na Wenyeviti kwa kuendesha kwa weledi mkubwa mjadala huu muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pongezi na shukrani kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini; Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi pamoja na Kamati nzima ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambayo wametupa ushirikiano mzuri na wa hali ya juu ambao umewezesha kazi yetu hii kuwa ya ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania waliochangia kwa maandishi, kwa kuongea na wale waliotoa ushauri wao katika kuonana na sisi ana kwa ana, kwani wamewezesha sana shughuli hii iweze kukamilika kikamilifu na niwaombe wananchi wa Tanzania watambue tu kwamba Wabunge wao wametoa michango yenye maana kubwa sana kwa Taifa letu pamoja na kwamba huenda nikawataja wachache, lakini wapiga kura wao wote watambue kwamba Wabunge wao wamechangia kwa hoja za msingi na zenye tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vile tu kwa wingi wao sitaweza kumtaja mmoja mmoja, kwa hiyo hata kama Mbunge wao

hatatajwa watambue kwamba wamechangia kwa hoja makini sana ni wingi wao tu hatuwezi kuwataja wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge 209 wamechangia na kati ya hao 206 wamechangia kwa kuongea na Wabunge watatu wamechangia kwa maandishi na kama nilivyotangulia kusema wengine wametupa ushauri wao kwa kuongea/kwa kujadiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kutoa ufafanuzi wa hoja zilizojitokeza; kati ya hoja ambazo kwenye mjadala zimejitokeza kwa kiwango kikubwa zilikuwa zinahusisha maeneo yale ambayo tuliweka tozo mpya.

Mheshimiwa Spika, la kwanza niwapongeze Wabunge kwa kuelewa hoja ya Serikali na umuhimu wa jambo lile ambalo tulikuwa tunaongea lugha moja ambalo kwa kiwango kikubwa Wabunge wenyewe walikuwa wameibua kwamba tunahitaji tuangalie kwa jicho la tofauti katika matatizo yanayojitokeza katika sekta zetu za muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kwanza ambayo tuliangalia kwa umakini mkubwa ilikuwa ni sehemu ya *TARURA,* barabara zetu na pili tulikuwa tumeangalia kuhusu upande wa maji, la tatu tulikuwa tumeangalia kuhusu upande wa elimu, la nne tulikuwa tumeangalia upande wa afya, miundombinu yake pamoja na mwelekeo wa kwenda kwenye *universal health care* na kipengele cha mwisho tulikuwa tumeongelea kuhusu miradi ya kimkakati ambayo ni miradi urithi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo tulikuwa tumependekeza ambayo kwa kiwango kikubwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania walitamani kupata ufafanuzi, moja ya eneo ilikuwa kuhusu makato ya kwenye simu upande wa muda wa maongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili kwa kiwango fulani lilikuwa halijaeleweka kile ambacho tulikuwa

tunakimaanisha, kuna wale ambao walikuwa wanadhania makato haya yanaenda kukatwa kwa idadi ya siku kwenye mwezi, kwa maana kwamba itahesabiwa kuanzia tarehe ya kwanza ya mwezi mpaka tarehe ya mwisho na kama hukuweka salio siku ukiweka unahesabiwa siku zote katika mwezi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ilikuwa inafananishwa kama ile ya nipige tafu ambayo kama jana hukuweka ama jana ulitumia kwa kukopa basi siku ukiweka inatakiwa ikatwe kwanza ile ambayo siku hiyo ilishapita. La hasha, sisi tulichopendekeza ni kwamba tumechukua takwimu za watumiaji wa simu, tukaweka makundi yao, kuna watumiaji wasiopungua milioni nane kwa viwango vya mwanzo ambao wana matumizi yao yasiozidi shilingi 1,000 inaenda inakuwa mpaka inafika wale wanaotumia shilingi 100,000 na kuendelea ambao wenyewe si wengi sana wako kwenye 60,000 naa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tulichoweka kwa wale watumiaji wanaotumia viwango vya chini kwa mfano anayetumia shilingi 1,000 na kwenda chini yeye atakatwa shilingi tano, na hiyo shilingi tano atakatwa pale alipoweka tu, kwa wale wanaotumia shilingi 7,500 hadi shilingi 10,000 atakatwa shilingi 76. Kwa wale wanaotumia shilingi 10,000 hadi shilingi 25,000 maana yake huyu inaweza ikawa ni mtu anayejiunga muda wa maongezi wa mwezi mzima kwamba ameweka kifurushi chake cha mwezi mzima kina *range* shilingi 10,000 mpaka shilingi 25,000; chukulia ni shilingi 25,000 kwamba ndicho anachojiunga nacho anakatwa shilingi 112; maana yake ni kwamba mwezi mzima amekatwa shilingi 112. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama anajiunga kwa shilingi 50,000 kwa mfano nani *Halotel* wana *bundle* linaitwa *Tanzanite* ambalo ukijiunga unaongea kwa mwezi mzima, chukulia ni shilingi 50,000; kwa hiyo kwa mwezi mzima anakuwa amekatwa shilingi 186; ni tofauti na ile hesabu tuliyokuwa tunapiga kwamba ni 200 kwa siku maana yake kwa mwezi ni shilingi 6,000 unaona hiyo tofauti kati ya shilingi 6,000

ambayo ilikuwa inatisha na shilingi 186 kwa mtu anayetumia shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema siku naweka hoja hapa mezani kwamba kwa kweli nachukia kuwapa Watanzania mzigo na kwa kweli nawahurumia Watanzania, lakini nikasema nawahurumia zaidi wanaojifungulia vichakani, kwa mtu anayeweza kutumia shilingi 50,000 kwa mazungumzo akichangia shilingi 180 ili kuokoa maisha ya mama zetu kuna shida gani kwa mwezi mzima! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mtu ambaye anaweza kutumia shilingi 25,000 ndio ni Mtanzania wa kawaida, akatumia shilingi 25,000 kwenye mazungumzo ndio ni Mtanzania na shilingi 100 ni kubwa, tukimuongezea kwenye matumizi yake ndio ni kubwa, mzigo, tunamhurumia, lakini shilingi 100 hiyo ikasaidia kupatikana vifaa tiba hospitalini, shilingi mia hiyo kwa mtu anayeweza kuongea kwa shilingi 25,000 kwa mwezi kwenye simu akasaidia tukapeleka vijana 21,000 waliokosa mkopo wa familia za kimaskini kuna shida gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo niendelee kutoa rai kwamba nchi hii itajengwa na Watanzania wenyewe, ni lazima tubebe majukumu hayo kama wazazi, lazima tubebe majukumu hayo kama Watanzania kwa sababu majukumu hayo ni yetu. Hata anayetumia shilingi 1,000 mpaka shilingi 5,000 katikati mle kuna shilingi 1,000 mpaka shilingi 2,500 anapoweka akichangia shilingi 10 halafu fedha ile ikaenda ikatusaidia upatikaji wa maji, kuna watoto wadogo wanabakwa wakiwa wanatafuta maji usiku ipo hiyo na sasa hivi imeongezeka na shida ya *corona* inayotuhitaji tuwane kwa hiyo kuna maisha yatapotea tusipokuwa na maji kwa jambo dogo tu la kunawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka vizuri haya matatizo ya maji tulipokuwa kule vijijini ilikuwa ikifika mwezi wa sita na kuendelea mpaka Krismas mnaanza kusoma nusu siku tu ili muende kutafuta maji. Sasa kwa umri wa nchi yetu

hivi si vitu vya kuviruhusu viendelee, vitakuwa vinapingana na hatua ya maendeleo tuliyoyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kuumia hiki kidole tukiwa tunachimba maji, hakijawahi kupata *shape,* hakijawahi kurudi kwenye hali yake ya kawaida, shida ya maji bado ni tatizo katika kila eneo. Kwa hiyo, hili na lenyewe tuliona tuifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo huu ndio mtiririko, tutaanza na shilingi tano na pale ni mtu anapoweka na itaenda inakuwa kufuatana na matumizi yake na mpaka inaenda hiyo shilingi 222 kwa wale ambao watatumia shilingi 100,000 na kuendelea na hili si jambo la kila siku, ni pale mtu anapotumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukirudi upande wa miamala; kwenye miamala tulienda kuzingatia hivyo hivyo kwamba nchi yetu ina matatizo, pamoja na jitihada kubwa ambazo zimefanyika, lakini kila hatua ya maendeleo unayoifanya itakuletea changamoto zaidi; ndio utaratibu wa maendeleo ulivyo, kila hatua ya maendeleo unayoifanya ndio inakuletea changamoto zaidi, kwa mfano, tunapoongelea kila kijiji kiwe na umeme, kila mtaa uwe na umeme, kila familia iwe na umeme, umeme ule sio nguzo na nyaya za umeme, tunahitaji chanzo cha kufua umeme kitakachotosheleza mahitaji ya nyumba kwa nyumba kwa nchi nzima kuwa na umeme. Vinginevyo tukiwekeza tu kwenye kusambaza nguzo yatakuwa makao ya kunguru tu wanapandapanda mmewaongezea miti, lazima tuwe na chanzo cha uhakika kitakachofua umeme kiweze kusambaza umeme katika maeneo hayo ndio maana tunasema kila familia lazima iwe na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tuna miradi ya kimkakati ambayo na yenyewe tukasema lazima tupate fedha na tukasema kama tutatafuta fedha kwa njia ya mikopo tu, tuna mzigo mkubwa Waheshimiwa Wabunge kwenye bwawa la umeme peke yake kwa muda huu ili

likamilike mpaka mwisho zimeshatumika trilioni kama mbili hivi bado tuna mzigo karibu trilioni nne.

Mheshimiwa Spika, ukitoka hapo ukiweka na reli, reli sio njia moja tu tunataka kuijenga, hii njia ambayo tunaondoka nayo, huu ni mwanzo kama alivyosema Waziri mwenye sekta, tuna na reli zingine Kusini, Kaskazini pamoja na yale matawi tukishafika Tabora mtawanyiko wake ule, ukipiga hesabu yake yote hiyo ni karibu dola bilioni 10 ambayo ni zaidi ya shilingi trilioni 22.

Mheshimiwa Spika, sasa fedha za aina hiyo ukisema tu uende ukakope zote tena uikamilishe kwa muda mfupi maana yake ni kwamba kwanza masharti tutakayopata hayatakuwa rafiki, lakini mbili mzigo utakalolibebesha Taifa utakuwa ni mzigo wa roho mbaya kwamba sisi tukope tu watakuja kulipa ambao hawajazaliwa, tutakuwa tunafanya kitendo ambacho vizazi vijavyo vitalaumu kizazi cha leo kwamba kama hawakutaka kujenga reli kwa nini wasingeacha tu tuje tujenge wenyewe uende tungekuja kukopa kwa masharti ambayo ni nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tumeona ni vyema tukafanya utaratibu wa kupata fedha kiasi tutapeleka kule wakati tunasubiri *credit rating* pamoja na taratibu zingine, lakini kwa wakati huo huo tuwe tunatafuta mikopo yenye masharti nafuu ambayo haitaipa mzigo mkubwa wa deni kwa Taifa letu ambao pia unaweza ukatusababisha tukaingia kwenye sifa mbaya za nchi zilizokopa kupita uwezo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hicho ndicho ambacho tulikizingatia kwa upande huo wa miamala na mimi niwaombe Watanzania kama nilivyosema tunazingatia mambo yanayotukabili mbele yetu na ndicho tulichofanya kuamua tukasema ni vyema tukafanya hivyo. Na kwa nini tuliona tufanye hivyo; mfumo wa kodi wa kwetu ulivyo ile *tax base* ilivyo mpaka hivi tunavyopanga bajeti ya leo ukiiondoa *indirect taxes* zile kodi ambazo kila mtu anaguswa kwa

matumizi ya bidhaa wale ambao wameandikishwa huo mzigo unaangukia kwa watu wachache.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mpaka sasa tunavyoonge walipa kodi wakubwa ni 504; ukienda walipa kodi walioandikishwa ni 3,162,000; sasa kama una walipakodi wakubwa 504 na walioandikishwa milioni tatu; una miradi inayohitaji shilingi trilioni 20 na kuendelea; karibu shilingi trilioni 24 hiyo hatujataja miradi mingine ambayo na yenyewe ni mikubwa, miradi kama ya madaraja, barabara za kuunganisha, hapo hatujaenda kwenye hizi za kimkakati tunazosema za kwenye vijiji vyetu ambavyo ni za muhimu sana, unawezaje kupeleka malipo haya yote yaangukie kwa hawa watu niliowataja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukasema kazi kujenga nchi yetu lazima ifanywe na Watanzania wote na Watanzania wajivunie kuijenga nchi yao. Kila Mtanzania anapoona jambo la maendeleo limefanyika ajivunie kwamba na mimi nimeshiriki, tukasema hii na yenyewe tushirikishe kwa upana wao, ndipo tulipoona tuanze kugusa awepo wa shilingi 10, shilingi 16, yupo wa shilingi 50, yupo wa shilingi 25, yupo wa shilingi 125, ukienda wa shilingi 30,000 ni shilingi 1,000 ukiienda shilingi 40,000 ni shilingi 1,500; ikaenda mpaka yule wa shilingi milioni tatu na kuendelea milioni tano, milioni 20, milioni 15 na kuendelea tukasema kwa kazi tuliyonayo kama Taifa kama unaweza ukawa na ukwasi wa milioni 15 tukichukua shilingi 10,000 kwako halafu ukajivunia kujenga nchi yako, kuna ubaya gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaingia kwenye rekodi ya kujenga nchi yako, unaingia kwenye rekodi ya kujenga nchi yako, sisi wengine huwa tunajivunia sana *lift* hizi kwamba inapojengwa reli unaingia kwenye kumbukumbu kwamba reli inajengwa ilikuwa umri wetu kama wazee wanavyotuambia kwamba wakati vita vya Kagera vinapigana mimi nilipeleka ng'ombe, wanajivunia wakati wa vita vya Iddi Amini mimi nilipeleka ng'ombe, mwingine anasema mimi nilipeleka mbuzi, wanajivunia wazee wetu,

hawakuwa matajiri wakubwa kihivyo, walikuwa matajiri wa moyo kwamba mimi nilipeleka mbuzi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine walikuwa na mabasi yalikuwa yanashusha abiria wa biashara wanabeba wanajeshi waende kupigana, ana-*sacrifice* fedha ambayo angeipata kwa biashara yake anapeleka basi liende kwenye ile vita. Sasa hivi hatuna vita za kiuvamizi, vita zilizosalia kwenye nchi zinazoendelea ni vita za kiuchumi kujenga mataifa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe na moyo wa aina hiyo kwa sababu hii nchi lazima iende na sisi tujivunie kwamba hapa lilifanyika hili tukiwepo, lilifanyika na hili tukiwepo, hebu fikirieni vijana wa rika langu, wakubwa zetu na wadogo zetu mnaofuatia, siku ikitokea katika kizazi chetu tukajenga reli zote za Kusini huku Mtwara kwenda kwenye maeneo ya uzalishaji, tukajenga Kaskazini huku kote, tukajenga na hizi kubwa tukasema hizi zilijengwa katika kizazi hiki, na Rais aliyekuwepo alikuwa Mama yetu Samia Suluhu, hili ni jambo la heri kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo tulivyowaza wenzenu, tukasema hii kazi lazima tuibebe wote, hivyo ndivyo tulivyofikia katika uamuzi huo na mimi naamini Watanzania tukikubaliana na mwenendo huu tutapiga hatua ambayo Tanzania itarudisha ile sifa iliyokuwa mbele inatajwa na kila mtu wakati wa ukombozi wa Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, makofi hayo hayatoshi kwa kweli, kabisa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, sasa tunachopendekeza, baada ya kuwa tumepata yale mapato nini tunapendekeza; tunapendekeza tupeleke shilingi bilioni 322 ziende kwenye maeneo yetu ambayo hayapitiki, hayana barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulishapitisha bajeti ya *TARURA* karibu shilingi bilioni 400 na sehemu, kama mnavyokumbuka.

Zile zitafanya ile kazi ya kawaida ya *spotting* na *periodic maintenance* kama ambavyo zilikuwa zinafanyika na zingine mgao ulishapita. Tunapendekeza tuongeze ziada ya zile shilingi bilioni 400 na bahati nzuri hiki chanzo kinakwenda moja kwa moja kwenye mfuko. Kwa hiyo, tutakapotumia zaidi maana yake makadirio haya yanaweza yakazidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende tukafungue maeneo ambayo hayapitiki. Mijini na vijijini tuna maeneo mpaka karne hii, nilisema na siku ile tuna eneo unakuta kijiji kina shule ya msingi, taasisi ya Serikali, ina zahanati, lakini hakuna gari inaweza ikafika pale. Hali ya aina hiyo haiendani na umri wa nchi yetu na heshima ya kiuchumi ambayo nchi yetu imetambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Jiji kubwa kama Dar es Salaam, nilikuwa naongea na Mbunge wa Kibamba akasema hata kwake kuna maeneo ambayo kwenye ramani yanaonekana kabisa yana mitaa, lakini hayapitiki. Sasa mtu anaishi Dar es Salaam, jiji kubwa ambalo linatambulika, lina mpaka *flyovers* halafu eneo lingine mlemle hata pikipiki haipiti, haya hayaendani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alisema jana kwamba tunaondoa miradi ile ya *DMDP* pamoja na *TACTIC,* muielewe vizuri. Tulichokuwa tunasema fedha hizi siyo za kwenda kwenye mapambo yale, kwamba wengine waendelee kubandika na kubandua halafu kwenye eneo lilelile pawe pana watu ambao hawajawahi kupata kitu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ile miradi itakuja, kama alivyosema Waziri, lakini alichomaanisha kwamba kuna maeneo yapo hayajafunguka kabisa, yapewe kipaumbele na haya yanakwenda kwenye majimbo yenu huko huko; awe Mbunge wa Dar es Salaam ana maeneo ya pale mjini na pembezoni; awe Mbunge wa kwenye miji ile 45, ana maeneo ya mjini na mle pembezoni. Kwa hiyo, hiki ndicho alichosema Waziri wa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tunakwenda kupata, ukiangalia kwenye hesabu, Wabunge na hapo ndiyo wapiga kura wenu waone kwamba walileta majembe kweli kweli; mnavyoondoka hapa kila mmoja ataondoka na siyo chini ya shilingi bilioni moja, inakwenda kwenye barabara hizo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, mkifuatilia hapa mtakuta kuna wakati *TARURA* ilikuwa inapata shilingi milioni 30, majimbo mengine yalikuwa yanapita kapa, mwaka mzima unapita. Sasa waambie wananchi wako kwa jinsi Mbunge ulivyo mjanja sasa hivi, umeishauri Serikali sikivu na ulivyopaza sauti mama yetu akasikia kilio chenu, na akasikia kilio cha wananchi wote, unakwenda kuondoka na siyo chini ya shilingi bilioni moja, iende kwenye kufungua barabara ambazo hazijawahi kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tukienda na utaratibu huu mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu tukaendelea nao kama walivyoanza *TANROADS,* walianza na kufungua mkoa mmoja mmoja na sisi tukianza hivyo hivyo tukafungua kijiji kwa kijiji, mtaa kwa mtaa, tutafika wakati hatutaongelea changarawe mitaa yote, tutaanza sasa kuwaza makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wengine wanadhani zile barabara kubwa za *TANROADS* za lami zinazounganisha mikoa zilikuwa hivyo hivyo, hawakusafiria yale mabasi yenye *carrier* juu. Mkipita mnavyofika mkishuka abiria na kondakta wote mko sawa, lakini tulianza na utaratibu huu huu na ndiyo maana tunasema Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Mungu amrehemu kule aliko, wakiwa wanakwenda na utaratibu huo wa mfuko na kuanza hatua kwa hata wakaenda, sasa hivi tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nchi ni kama ujenzi wa nyumba, kuna anayejenga msingi, kuna anayejenga kuta, kuta anayepaua, kuna anayeweka marumaru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza na tumeongea na wenzetu wa Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, tumeongea naye na wataalam wake na

wametuambia wanafunzi 11,000 waliokosa mikopo mwaka jana na wa mwaka huu walikadiriwa kama 10,000; ni kama *21,000 plus,* mahitaji ya fedha ni shilingi bilioni 70. Kwenye shilingi bilioni 500 ambayo tulishapeleka tunaongeza shilingi bilioni 70 ziende ziwapeleke watoto wa mwaka jana...*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haleluya!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hapa hujaeleweka, hebu rudia kidogo, maana yake Wabunge wengine naona kama hawajaipata hii vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, mwaka jana walikosa mikopo takribani watoto 11,000 wale ambao wana *admission,* wamepokelewa na vyuo kwamba wana sifa za kuingia vyuoni, lakini walikosa masomo kwa sababu walikosa mkopo na wazazi wao hawana uwezo, wengine hawana wazazi na wakabaki majumbani 11,000. Na wanakadiriwa mwaka huu tena wangekosa 10,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwenye familia zetu mtoto ambaye amefaulu mtihani huwa inakuwa faraja ya familia na ukoo mzima. Ikitokea amekosa mkopo, siyo fedha ya msaada, mkopo, inaleta majonzi kwenye familia na ukoo mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapendekeza kuongeza kwenye bilioni tulizopitisha kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, shilingi bilioni takribani 500, tunaongeza shilingi bilioni 70 ambazo zinakwenda sambamba kuwapeleka watoto wote. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haleluya!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ummy Nderiananga aliongelea upande wa wanafunzi wenye ulemavu; tumepokea mapendekezo yako

na tunaendelea kuyafanyia kazi Kiserikali, tutajua kwenye utekelezaji wake kuhusu wanafunzi wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kwa upande wa maboma ya elimu, kama tusipopanga kuanzia sasa kule tunakokwenda watoto wetu watapata sifa za kuingia shuleni, lakini hawatakwenda kwa sababu kuanzia mwaka kesho tunakwenda kupata toleo la kwanza la wale wanafunzi walioandikishwa kwa elimu bila malipo shule ya msingi, darasa la kwanza, ndiyo wanakwenda kumaliza darasa la saba na wanatakiwa waanze kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, tusipojipanga kwenye miundombinu kuanzia sasa takwimu zinaonesha tutakuwa na uhitaji wa vyumba vya madarasa wa kiwango cha juu sana na hatutaweza kufanya kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka, bahati nzuri wewe ni kaka yetu tulio wengi hapa, utakumbuka zamani kwa ajili tu ya kukosekana miundombinu watu ni hawa hawa, Watanzania ni hawahawa na akili zao ni hizihizi, lakini ilikuwa inatokea kijiji kizima, darasa lenye watu sitini, mia, inatoka kapa. Mnaambiwa tu wamefaulu 50 lakini hawakuchaguliwa, maana yake wakichaguliwa wanakwenda wapi, ndivyo ilivyokuwa. Mimi nakumbuka hata Mazengo tulikwenda watano.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi tulivyojenga shule kwenye kila kata mmeona wanaobaki wameendelea kuwa kidogo sana. Maana yake nini; wana pa kwenda na kule kule wanakokwenda ili muone kwamba akili wanazo, wanapata *division one* kule kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna rika hapa la enzi ya wamefaulu ila hawakuchaguliwa, kuna rika la watu wana akili sana na wangelitumikia Taifa, hawakwenda kwa sababu ya nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hata sasa kuna baadhi ya mikoa kwa sababu bado tunagawanya chumba kimoja

tunaweka ubao katikati, watoto wengine waangalie ubao mmoja wengine waangalie mwingine; kwa hiyo, mikoa ile ikitokea ametokea mtoro amekwenda kuchunga kama tulivyokuwa tunachunga wengine, hata hawahangaiki kumtafuta kwa sababu wanajua ametupunguzia na kero ya madawati huyu, ametupunguzia na mbanano. Tumefanya suala la elimu liwe la kuviziana kwa sababu miundombinu haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tunaoshughulika na mipango tunaona hili jambo tunaweza tusilimalize mara moja, lakini ni vyema tukaanza kupanga haya mambo tunakokwenda. Uamuzi wa maeneo mengi tunaufanya kwa kuviziana kufuatana na miundombinu iliyopo na ndiyo maana familia tulizokuwa tumezaliwa watoto kumi au 11 hatukuwa tunafanya *birthday,* utakumbuka *birthdays* ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata kwenye masuala ya miundombinu, uamuzi wa kupeleka watoto shuleni miundombinu inachangia. Hata haya mambo tumebishana ya waliopata ujauzito warudi ama wasirudi, unaweza ukakuta uamuzi unakuwa *shaped* na wakirudi wanakwenda wapi. Tunafanya kuviziana kwa sababu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la elimu linatakiwa liwe wazi tu, hata ukitaka kusoma lini wewe soma, si tunataka upate akili, upate uelewa? Mbona elimu ya watu wazima tuliwasomesha wazee, tulisomesha na wana wajukuu. Kwa hiyo, tumeona lazima tushughulike na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nini tunachopendekeza; tunapendekeza tuanze na maboma 10,000 ambapo tunapendekeza tupeleke shilingi bilioni 125 kwenye upande wa maboma na hapa kila Halmashauri mtaondoka na maboma yasiyopungua kumi kwenye maeneo yenu ili kila mmoja aweze kwenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tutakapoenda kwa mwaka hadi mwaka tunakwenda kuyamaliza na yenyewe na hapo yatakwenda juu zaidi kufuatana na mchanganuo wa

gharama halisi utakavyoonekana kwenye fedha hizi ambazo tumeweka za nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye maboma ya afya; tuna maboma tulikuwa tumetengeneza, kuna zahanati na kuna zahanati zile zilizoko kwenye kata. Tuna zahanati ziko kwenye kila kijiji na tuna zingine tumeziweka kwenye kata, hii ni tofauti na vile vituo vikubwa ambavyo tunaviweka vina *facilities* nyingi. Vilishajengwa vingine vina miaka kumi, vingine 15 na hii ilikuwa nguvu ya wananchi. Tunapendekeza tupeleke shilingi bilioni 100 kwa ajili ya eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye haya maboma ya afya tunapendekeza tuyafanyie kazi kwa sababu hiki tunachoendea mbele cha bima ya afya kwa wote, hiyo bima ya afya kwa wote siyo ile kadi, ni *facilities* (vitendea kazi) ambapo inaanza na hospitali zenyewe, lakini pia dawa pamoja na vifaa tiba ambavyo vinatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima tukamilishe kwanza haya yapatikane kila eneo na tunaendelea kufanya tathmini, wenzetu wa TAMISEMI wanaendelea kufanya tathmini na maeneo yale ambayo ni ya tarafa ama maeneo ya kimkakati ambayo hayajapata vituo vya aina hiyo. Lakini sambamba na yale ambayo yanahitaji ukamilishwaji ambayo tayari kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu aliposema kazi iendelee na kazi inaendelea, alikuwa anamaanisha hivyo. Hapatakuwepo na sehemu pana *gap* ya kazi inayotakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hilo hilo la afya kwenye bima ya afya kwa wote na hospitali hizi ambazo zinaangukia Wizara ya Afya, tunapendekeza tupeleke shilingi bilioni 50 kwa ajili ya vifaa tiba pamoja na dawa, na hii ni nyongeza ya fedha ambazo zilishatolewa kwenye bajeti mama ya sekta ambayo tuliipitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja za Wabunge, jambo moja ambalo lilisemewa kwa sauti kubwa sana na kwa msisitizo sana, lilikuwa jambo la *ring fencing* ya fedha hizi. Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanataka kujiridhisha kwamba fedha hizi zitatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja, niwahakikishie Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais yuko makini sana kwenye masuala haya ya fedha, sana. Sisi tulioko kwenye Wizara ya Fedha anatuelekeza kila wakati kuhakikisha fedha zinakwenda kwenye maeneo yaliyokusudiwa na maeneo yenye tija kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaifafanua zaidi tutakapokuwa tunaongelea masuala ya siku 100; lakini niwaelezee tu kwamba Serikali iko makini kwenye jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwenye hili ambalo Waheshimiwa Wabunge mmelisema kwa nguvu sana, nilikuwa nawaona Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Lucy, Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Nape pamoja Wabunge wengine wengi, ni vile tu siwezi kumtaja kila mmoja, mlisema sana tuwahakikishie kwamba fedha hizi zitakuwa *ring fenced. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi niseme mbele yako, kwa sababu sekta hizi tunazozipelekea fedha nyingi zina mfuko, wala hatukuona sababu ya kuanzisha mfuko kwa sababu tumekitaja chanzo na tukataja zinapokwenda. Maana yake zinatoka kwenye chanzo, zinakwenda moja kwa moja kwenye mfuko ule ambao upo.

Mheshimiwa Spika, nimeshaeleza maeneo mengine, nilikuwa bado sijaelezea upande wa maji. Maji tulishapeleka bajeti. Muda huu ambapo tumeweka nyongeza hii tuliyoomba kwa Bunge lako Tukufu, tunapendekeza tuwapelekee Wizara ya Maji shilingi bilioni 207 za nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kama alivyosema Mheshimiwa Maganga jana, kwamba yeye ile fedha ya *TARURA* anatamani anunue greda; na mimi naendelea kuungana naye na ninamshauri Waziri wa Maji, fedha nyingine wanunue magari ya kuchimba visima, nyingine wanunue magreda ya kuchimba mabwawa, halafu fedha nyingine twende kwenye utaratibu wa kisima kila kijiji. Kama umeme upo kila kijiji tunakosaje kisima kila kijiji? Hili ni jambo ambalo litaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo Mfuko wa *TARURA* upo kisheria, hivi tunavyoongea, na chanzo tumekitaja. Maana yake fedha itatoka kwenye chanzo inakwenda kwenye Mfuko wa *TARURA* kama ambavyo fedha zile zilizokuwa zinakwenda kwenye *TARURA* zimetumika zilivyokusudiwa kwa sababu kuna Mfuko wa *TARURA. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Mfuko wa Maji; fedha tulizotaja kutoka kwenye chanzo zinakwenda kwenye Mfuko wa Maji. Tuna Mfuko wa Elimu ya Juu, Bodi ya Mikopo, fedha iliyotajwa inakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bima ya afya kwa wote sheria inakuja siyo siku nyingi, kwa hiyo, hatukuona kutengeneza sheria inayohusu tu huo mfuko wakati kuna jambo linakuja kubwa linalohusisha bima ya afya kwa wote. Kwa maana hiyo na mfuko wake utatajwa na sheria ambayo itakuja kufuatana na mpangilio unavyopangwa wa shughuli zetu za Kibunge *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa maboma, hiyo kwa sababu ni maboma, ni kitu endelevu, tumeona yenyewe itakuwa fedha ambayo inakwenda kwenye Wizara husika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, *SGR* pamoja na reli, Mfuko wa Reli upo, kwenye *SGR* ni mradi wa kimkakati ambao wote tunautolea macho kwamba ni lazima ukamilike. Kwa hiyo, tumeona kwa kweli Wabunge pamoja na Watanzania

mtuamini kwenye hili, tunakwenda kulifanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TARURA* tunarekebisha kipengele kile ambacho kilikuwa kinazuia Halmashauri, Majiji na Manispaa kutengeneza barabara. Kama tumeshachukua baadhi ya mzigo wa kuwalipa Madiwani kwenye makusanyo yao ya ndani tunafungulia kanuni ile na wenyewe waweze kufanya *periodic maintenance* ya barabara zao. Kwa hiyo hilo tutalifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ninaamini tuna majiji ambayo wana uwezo mkubwa kabisa wa kuweza kuzitengeneza barabara zao na tukaunganisha nguvu hii ambayo tumeisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilichangiwa kwa hisia na Waheshimiwa Wabunge na kule kwa wananchi wetu lilikuwa na hisia, ni jambo la kodi ya majengo kwa kutumia LUKU. Kati ya maswali yaliyokuwa yanaulizwa ni inakuaje mpangaji ndio awe mlipaji? Je, nyumba zenye mita nyingi? Nyumba kubwa zenye mita moja? Itakuaje kwa nyumba ya nyasi? Itakuaje kwa nyumba za vijijini; itakuaje kwa nyumba zisizo na umeme; taasisi pamoja na rika lililosamehewa itakuaje?

Mheshimiwa Spika, moja niwaombe Watanzania tusiigope teknolojia, teknolojia imekuja ili itusaidie, duniani kote teknolojia imeletwa ili kurahisha ufanyaji wa mambo, ndiyo kazi moja kubwa ambayo unaweza ukaitaja kwa sentensi ya ujumla, imekuja kurahisisha kazi. Sasa wenzetu ambao wanashughulika na masuala ya umeme pamoja na wale wanaoshughulika na *IT* wametuhakikisha kwamba mambo haya yote yanakwenda kwa *programming.*

Mheshimiwa Spika, leo hii hata tulivyoongea na Waziri wa Nishati walituhakikishia kwamba wanao uwezo wa kuitisha LUKU zote, wanao uwezo wa kuitisha mita zote, wakajua na mtumiaji anatumia kiwango gani, wanajua, wanajua hata

*trend* ya matumizi wanajua, wanajua na nyumba zenye mita zaidi ya moja, hazikujibandika zile mita zimeenda kuwekwa.

Mheshimiwa Spika, takwimu zake zote zipo na zipo namna ya kuitisha, tulivyohakikishiwa hayo tukaona ni jambo ambalo tutafanya *programming* na wenzetu hivi wapo *busy* wanafanya *programming.* Watafanya *programming* tunaitoa sheria nzima ile iliyokuwa inatumika kukusanya *manually* tunaipeleka tukusanye kiteknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuendi kuvunja Torati, tunaenda kuimarisha Torati, vilevile ilivyokuwa inafanyika *manually* tunaipeleka tunaikusanya kiteknolojia, kwa mfano, kama jengo moja ambalo linastahili kuwa la mita moja lina mita 12 tunaenda kuzi-*program* kwamba zipo 12; kwa hiyo, kwenye 12,000 tunagawanya kwa 12 tunazi-*program* kwa hiyo kwa mwezi atakuwa analipa mia, mia badala ya 1000 ni 12 gawanya kwa watu 12. Tunagawanya kwa idadi ya mita tupate ka kiwango ambacho kwenye kila kijimita tutapata.

Mheshimiwa Spika, wengine walikuwa wanasema je, wale ambao hawatumiagi hata shilingi 1,000 hiyo kwa mwezi, wenzetu kimtandao unaitisha wale ambao hawatumiagi hata hiyo maana yake unawatoa kiurahisi kuliko kutembea siku nzima unawatafuta. Unaitisha tu au una *blacklist* hawapo na wale waliosamehewa hivyo hivyo una *program* unawatoa, hivyo hivyo na kwenye nyumba ambayo ina mita zaidi ya moja na kwenye eneo lilitakiwa kuwa na mita zaidi moja mathalani ghorofa lilitakiwa kuwa na malipo yanayoendana na *flats* zile ilivyokuwa imebainishwa kwenye sheria tuna *program* hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tuliona hii imerahisisha utaratibu kwa wananchi wetu ni wao tu kukubaliana na hali hiyo na waweze kujua kwamba teknolojia imekuja iturahisishie. Hebu fikiria uwezekano katika karne hii eti watu wanatangaziwa *deadline* ya kulipa mita unakuta wamepangana mstari kama hapa na Dodoma Sekondari kule, wanaenda kulipa shilingi 10,000; mwingine ametoka sijui wapi anapanda gari, mwingine anatumia nauli, mwingine

anaendesha gari, mwingine anapoteza na muda anaenda kulipa shilingi 10,000, anaenda kulipa shilingi 50,000 tumezigawanya kama tulivyozigawanya, tuna *program,* zitakuwa *programmed* hivyo ndivyo ambavyo itafanyika, hivi vitu vinawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa wale waliokuwa wanapata msamaha kama ni wazee, kama ni Taasisi za Kidini tunaenda kufanya hivyo hivyo, tuna *program* kwenye vitendea kazi vyetu hawatakuwepo na tunaenda kutekeleza sheria vilevile. *(Makofi)*

Kwa nyumba zile ambazo zipo vijijini wengine walikuwa wanabandika tu kanyumba kapo kijijini hapana, hii hatutaenda kutoza kwenye kila mwenye umeme na wala hatutaenda kutoza kwa matumizi ya umeme kwa sababu tukitoza kwa matumizi ya umeme tutaongeza gharama za uzalishaji, tunaenda ku-*program* kodi inayotakiwa kutozwa ya jengo kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Spika, nchi zote zilizoendelea hawatozi kwa kupanga mistari, wanatoza kieletroniki hiyo ndiyo faida ya teknolojia. Hata hapa Afrika, Namibia kuanzia kodi ya ardhi wanatoza kwa utaratibu wa LUKU, kodi ya jengo wanatoza kwa utaratibu wa LUKU, kwa hiyo mtu anakuwa anajua kwamba nina *commitment* zangu hizi hapa anazitoa kwa kutumia simu yake akiwa yupo nyumbani kwake, akiwa yupo ofisini kwake bila kusumbuana kupanga foleni kwa njia zile za kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata maeneo ambayo yatatozwa ni yaleyale yaliyoanishwa yenye sifa siyo kila kijiji, siyo kila nyasi, siyo kila mwenye umeme ni yule ambaye anaangukia kwenye sifa zile ambazo tulishakubaliana kisheria. *(Makofi)*

Kwa wale wachache ambao wanatumia *solar* hili eneo tumesema ni wachache wale wataendelea ku-*graduate* kuungana na wale wenye umeme, tumewaachia TAMISEMI watafanya hiyo na kitakuwa moja ya chanzo

ambacho na wenyewe watatumia kwenye haya maeneo mengine ambayo tunawakabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa linasemwa kwamba sasa je, kwa nini itozwe kwa mpangaji? Nasema na nasisitiza kodi hii si ya mpangaji, hii ni kodi ya mmiliki, hii si kodi ya mpangaji ni kodi ya mmiliki, utaratibu huu tunaotumia ni utaratibu ambao hata kwa karatasi alikuwa akikutwa yule ambaye anaishi kwenye ile nyumba anasaini kwa niaba ya mwenye nyumba, wakionana kwa taratibu wanazozijua wana-*offset* hiyo *difference* hata kwa karatasi ndivyo walivyokuwa wanafanya, ndiyo utaratibu uliokuwa unafanyika, hakuna nyumba ambayo ina mita ambayo haihusiani kabisa na mwenye nyumba na hakuna nyumba ambayo mtu anaishi hausiani kabisa yaani hawajuani wala hawajahi kuwasiliana hata kwa kutumia mtu wa kati kama dalali kwamba wewe basi kaa hapa, hakuna mtu anayeenda kuingia tu kwenye nyumba isimekane kwamba hata muona wala hawatakuwepo na hata *third* ya *part* wa kuonesha huyu anakutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hoja ya kwamba akitokea mwenye nyumba asiye na busara au akatokea aliyemkorofi, niwatangazie wenye nyumba wote hili si jambo la mahusiano, hili si jambo la mahusiano ya mpangaji na mwenye nyumba wala hili si jambo la kirafiki hili ni jambo la nchi, jambo la sheria, akitokea mkorofi nchi hii haijawahi kushindwa kushughulika na wakorofi, akitokea asiye na busara pia na yenyewe tutafundishana busara hili ni jambo la nchi ni jambo la sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo wapangaji wala wasipate shida, kama una mwenye nyumba ambaye atakiuka sheria za nchi zinazohusu masuala ya kodi sheria zetu zipo wazi kwa watu wa aina hiyo ni kitu gani kinafanyika kwa maana hiyo hatua za kisheria kwa watu wa aina hiyo zitafuata tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona hili na lenyewe nilisisitize na niwaombe Watanzania tusiogope teknolojia, tutumie

teknolojia itusaidie kuendesha mambo yetu kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa hapa kwenye hilo la upande wa kukusanya; watu wameanza kuchanganya hii habari ya kulipa kodi. Tunaposema kulipa kodi kwa hiari watu wameanza kuchanganya wanadhania kodi ni hiari, tunaposema tutoe elimu watu walipe kodi kwa hiari watu wameshaanza kuchanganya wakidhani kodi ni hiari na wengine wanachanganya halali na hiari, kana kwamba sasa mtu atakuwa na uamuzi wa kulipa ama kutokulipa kwamba anaweza kupanga tu kwamba yaani anaambiwa kabisa kodi yake stahiki ni hii ila anapanga kama alipe au asilipe, *that is a gross mistake. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kodi yoyote anayostahili mtu kulipa ni kitu cha lazima, lazima alipe. Tunachosema kwa hiari tunasema usisubiri kusukumwa, tunaongelea wajibu kwamba watu wawajibike kulipa, watu wanataka kuchanganya hiari aone kama vile anaweza akawa na uamuzi wa kulipa ama kutokulipa. Si jambo la kuamua ama ulipe ama kutokulipa, kodi stahiki kwa mtu yeyote kodi stahiki lazima alipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachosema tutatoa elimu tunasema usisubiri kusukumwa na wala usiingie kwenye mitego ya kukwepa kulipa unatafuta matatizo, hivi tunavyoongea tunapoanza Julai, tutafuatilia utaratibu wa matumizi ya *EFD,* tutayafuatlia sana lakini pia tutafuatilia watu walipe kodi stahiki, tutafuatilia sana watu walipe kodi stahiki, tutalifuatilia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wale ambao wanapenda kuamua kwamba nipewe bei isiyo na risiti au yenye risiti twendeni tutoke kwenye kupeana bei yenye risiti au isiyo na risiti twendeni bei ni moja yenye risiti lipa kodi ya Serikali. Tutaelimishana kwenye hili na wakati ule nilimteua unajua kuteua ni kuzuri, nilimteua Subira natamani kulirudia hili neno nilimteua Balozi wa Kutoa Elimu ya Kulipa Kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafanya na teuzi zingine namteua na Zulfa Omary kutoka Pemba na yeye atatusaidia...*(Makofi)*

**SPIKA:** Yupo wapi Mheshimiwa Zulfa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, namteua na Ndugu yangu Ameir Abdalla Ameir yule shabiki mpya wa Yanga ambaye aliguswa na bajeti hii, haukuwepo siku ile kwenye kiti, Mheshimiwa Ameir alisema tangu ujana wake, tangu mtoto kwa takribani zaidi ya miaka 12 iliyopita alikuwa shabiki wa Simba ila anasema kwa bajeti hii ameamua kuingia Yanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hii elimu pia ya mlipa kodi, si elimu ya darasani tu, kule tunapata elimu ya darasani, lakini pia tunataka tufanye elimu ya hamasa ya kuhamasishana, taasisi yangu ya Mamlaka ya Mapato watafundisha kitaalamu *technical issues* pamoja na faida zile, wataonesha na kinachofanikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini, vijana wetu pia wana lugha wanazoelewana wao wenyewe, kwa hiyo na kule nateua kwenye kundi hilo, nateua mabalozi wa kuhamasisha kulipa kodi kwa hiari, namteua mwana kabumbu mashuhuri Mbwana Samatta na yeye awepo kwenye Mabalozi ya Kulipa Kodi, namteua Ndugu Edo Kumwembe na yeye awepo kwenye Mabalozi ya Kulipa Kodi na kwa wanawake namteua Ndugu Hamisa Mobetto na yeye atatusaidia kuhamasisha kwenye walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tulikuwa tunapata shida nalo ambalo na lenyewe tunalifanyia kazi kama Serikali na kama Wizara, tuna tatizo kwenye masuala ya ukadiriaji, tunashida kubwa kwenye masuala ya ukadiriaji, ndiyo maana tuna mrundikano mkubwa sana wa kesi kwenye vyombo vyetu.

Mheshimiwa Spika, wanauliza huku hamna balozi? Subirini nimemteua Matiko kuwa Balozi wa Usemaji upande wa Magereza. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri bado sijaisikia vizuri hii. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nimemteua Esther Matiko Msemaji wa upande wa Magereza. (*Kicheko)*

**SPIKA:** Ana uzoefu wa kutosha. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MAPINGO:** Mheshimiwa Spika, na nimemteua Mheshimiwa Ester Bulaya upande wa masuala ya wastaafu, amelisemea sana hilo pamoja na wenzake na Mheshimiwa Cecilia upande wa mfumuko wa bei, hizo hoja zilikuwa zinakuja huku mbele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, kwenye upande wa ukadiriaji kuna shida moja tu sisi kama Serikali tumeiona. Moja; ukadiriaji ile ya kwamba mimi nakukadiria, usiporidhika kesho uje tuongee na mimi mwenyewe na usiporidhika nenda kwenye hatua nyingine, lakini ili usikilizwe huko unapokwenda ulipe kwanza theluthi moja ya kile ambacho umekikataa.

Mheshimiwa Spika, hivi theluthi moja ya bilioni 150 ni ngapi? Theluthi moja ya bilioni 90 ni ngapi? Sasa tunapendekeza tunapokwenda tutaanzisha chombo cha Msuluhishi wa Masuala ya Kikodi ili kuwatengenezea watu wetu badala ya kutumia njia moja ya kupeleka kwenye Mahakama ya Kikodi pamoja na *bureau* za kikodi wawe na fursa ya kusemea mambo yao, lakini pia tunaendelea kuimarisha ile mifumo ya ndani ili pasiwe na uonevu kwenye ukadiriaji wa kodi mtu akadiriwe kodi anayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 1 Julai hili na lenyewe tutalifuatilia kwa karibu sana. Kwa mfano nilipata kesi moja hivi juzi, kuna mtu mmoja aliendа akakadiriwa shilingi milioni 400, alivyokadiriwa shilingi milioni 400 yule aliyemkadiria akamwambia alete shilingi milioni 200 za kwao wale wakadiriaji, akakataa, alivyokataa hiyo ilikuwa tarehe 23 Novemba, akakataa kutoa shilingi milioni 200 hiyo alivyokataa, tarehe 23 Novemba alivyokadiriwa kwa barua kwamba makadirio yako ni shilingi milioni 400, lakini

akaambiwa lete shilingi milioni 200 alivyosumbuka sumbuka akaambiwa wewe unajifanya mjanja. Tarehe 27 kutoka tarehe 23 Novemba siku nne baadaye akakadiriwa shilingi bilioni 2.5, hiyo ni tarehe 27 Novemba 2020, alivyokadiriwa hii sasa kaenda akaongea nao kwamba ule mpango basi nimeshakubali akatanguliza shilingi milioni 100, alivyotanguliza shilingi milioni 100 tarehe 3 Disemba ikashushwa ile kutoka shilingi bilioni 2.5 ikarudi shilingi milioni 320. Maana yake nini? Maana yake hii ni rushwa, haya hayawezi yakawa makosa ya kawaida. Nimepeleka kumbukumbu hii vyombo vya dola vitachukua kazi yake na wale watu nimemuelekeza Kamshina achukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dakika zangu zimekwenda, nilipokea jambo lile alilisemea Mheshimiwa Nape la kule *TIPER,* nimeelekeza zoezi lile liendelee, waendelee na utaratibu, kulikuwepo na shida ya taratibu zetu za kindani ya kiofisi nimeshaelekeza waendelee hizo hatua zingine ambazo zilikuwa zinakwamisha zitakuta wale kule wanaendelea pasiwe na *gap* pale.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Ma-*VEO,* pamoja na posho mlizotaka za Madiwani ziongezeke za Watendaji niwaombe mridhie tumeanza na hatua hii, na kama ambavyo Mheshimiwa Rais alisema kwa wafanyakazi wote, alisema tunaanza na hatua hizi mwaka kesho tutaangalia zaidi na mimi nitumie kauli ile ile aliyoisema Mheshimiwa Rais tuanze na hatua hizo halafu mwaka kesho tutaangalia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, kilimo na uvuvi, tumeshaongea na Wizara zinazohusika na mimi natoa ridhaa ya yale maeneo ambayo yanataka kufanya *financing* za kisasa wafanye hivyo kwa upande wa mifugo, kilimo na uvuvi na sisi kama Wizara tutafanya nao karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kwa upande wa Zimamoto, upande wa Zimamoto tumeongea na Waziri anayehusika natoa ridhaa arekebishe kanuni kwenye upande wa makato

yale ya tozo zile ambazo zinakuwa ngumu kukusanyika kwa upande wa Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Askari Magereza pamoja na wa Zimamoto na yenyewe tunaoanisha, tumeongea na Waziri mwenye sekta, Mheshimiwa Simbachawene, tumeoanisha na wenyewe kwenda miaka sita kama tulivyosema kwa polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mambo ya sensa ya mwaka huu inayokuja tunapanga tuimarishe na kile kipengele cha makazi, tulikuwa tunaangalia zaidi upande wa idadi ya watu, tutaweka mkazo kwenye upande wa makazi ili hivi vitu vingine ambavyo vinahusiana na mambo ya makazi na vyenyewe viweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya kimikakati, Mheshimiwa Asenga amesema sana kule kwake, nimemuelekeza Katibu Mkuu ashungulikie yale maoni yako, asimamishe lile jambo ambalo lililokuwa linafanyika ambalo umelisema kwa nguvu sana ili waweze kuingia kwenye mkataba ambao utakuwa na manufaa kwa wananchi siyo ule ambao unaleta fedha, unatumia fedha nyingi kuliko maeneo mengine yote ambayo yaliwahi kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa *Covid* tunaenda na utaratibu ambao Mheshimiwa Rais aliunda Kamati na kamati ile ilishatoa taarifa na sisi tutaendelea kufanya kama ambavyo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengine tutaendelea kufafanua tunapokuja kwenye *Finance Bill,* lakini nililisikia jambo la Mheshimiwa Festo Sanga la nyasi wamesema na Wabunge wengine wengi ambao wamesema kwa kweli isiishie tu majiji na sisi tunakubaliana, tutaenda mpaka Manispaa na kwa maeneo mahususi ambayo hayako Manispaa wala hayako, lakini yanauwitaji huo tutaweka kipengele ambacho itahiji ruhusa maalumu mbali na ile ya BMT ambayo mlipendekeza tuipeleke ya kutolea ridhaa ili iweze kuombewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutaenda mpaka Manispaa, lakini kama kuna eneo mahususi litaombewa tutaweka kwenye kipengele tunavyokuja kwenye *Finance Bill* kwa yale ambayo hayako pale, tumeona tuanze na hivyo kwa ajili ya *control,* hilo lilikuwa na nyasi bandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona kengele imeshagongwa kwa kumalizia, tumeongelea hii sekta ya michezo, lakini lazima kwenye michezo mimi ninavyoangalia hii naongea tu kiuanamichezo, siyo kama shabiki na uniazime dakika zingine mbili za nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye michezo bado tunakosea kwenye mipangilio/mipango yetu, vitu vyetu vingi bado vinakuja kwa dharura. Ninaposema haya kwanza niipongeze kabisa Simba imefanya hatua kubwa sana mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nilivyokuwa naiangalia Simba ya mwaka huu, Simba ya mwaka huu ilikuwa ya kwenda kuchukua ubingwa. Kuna mahali tumekosea na tunakosea pale ambapo hatuweki vipaumbele, yaani sisi kwetu mambo yote yako sawa tu, kwamba mtu anaenda kucheza mchezo ambao unaweza kuleta kombe Tanzania kwa mara ya kwanza, anaenda kucheza nusu fainali, maana yake ili ucheze fainali lazima ucheze nusu fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anaenda kucheza mchezo mkubwa wa kuleta kombe mathalani, ukishinda nusu fainali na kiwango nilichokuwa nakiona wangeweza kuleta kombe. Huku una mchezo wa nusu fainali wa muhimu kwenye historia, katikati yake unaweka mechi ya watani. *(Kicheko)*

Sasa mimi nilivyoona Simba walivyofungwa kule Afrika Kusini, wao na wengine wanaaminishwa kama wamehujumiwa na nani yule/anaitwa nani yule, Senzo, wengine wanaaminishwa kwamba wamehujumiwa na watani mnawalaumu watani bure. Kiuanamichezo kabisa tunakosa mpango, Simba imeenda kucheza *South Africa* bila *game plan,* yenyewe ilijiandaa na mechi ya mtani na mimi

niwapongeze Yanga, walivyoenda uwanjani wakakaa dakika kadhaa wakaona Simba hawapo, wakajua wanajiandaa na mchezo hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, *on a serious note* timu zinazokwenda kwenye mashindano ya Kimataifa, zinaleta sifa ya Taifa. Lazima bodi hizi zinazosimamia wawe wanawapa kakipaumbele wawape, waangalie wangeweza kupeleka mchezo huko. Kwa sababu leo hii, kwenye timu zetu hata kama ni fainali ukiweka mtani hapa akili zote na miundombinu yote inaelekea hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Simba hii ilivyokuwa imempiga Al-Ahly ingehujumiwa na Senzo kweli! Eti ihujumiwe na mashabiki! Hapa walienda bila *game plan. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, la mwisho niwapongeze sana wana Yanga ambao wamewaunga mkono Simba. Wamewaunga mkono Simba, wana Yanga wamewaunga mkono Simba kwa kuwapa Morrison, licha ya wana Simba kuwa na mashabiki wenye heshima wengine tunao humu humu, hawakuwahi kurudisha hata tiketi tu ambayo Yanga walimletea Morrison hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nakukumbusha baada ya hapa kuna kura zinapigwa! *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wana Yanga muendelee na upendo huo huo na wala waachieni tu Morrison anakuja Makambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimewasilisha na kufafanua baadhi ya hoja, msingi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022, 2025/2026, wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, kwa mara nyingine tena nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote, wananchi na wadau wote kwa kuendelea kushirikiana pamoja katika kutekeleza mpango huo. Na niwaombe Watanzania wote tujitoe tumuunge mkono Rais wetu katika kutekeleza dira hii twende

naye bega kwa bega nchi hii itajengwa na Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru tena, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuiunga mkono Serikali na kabla sijahitimisha maelezo yangu, nichukue fursa hii pia niwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, nikianza na Naibu Waziri - Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni, Mbunge na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu Emmanuel Mpawe Tutuba, Naibu Makatibu Wakuu - Ndugu Amina Shaban, Dkt. Hatibu Kazungu na Ndugu yangu Adolf Ndunguru kwa kutupa ushirikiano mkubwa katika kuandaa na kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Niishukuru tena Kamati yako ya Bajeti nimeenda mle hii Kamati inafanya mambo *very professional*, tulifanya uchambuzi ulio bora sana na ndio maana kazi yetu inakuwa rahisi. Naamini tutatekeleza pakubwa zaidi na hata zile hoja walizotoa za kutengeneza utaratibu wa *monitoring and evaluation,* unaweza pia ukaendelea kuzitumia Kamati hizi. Kamati ya Bajeti, ya *LAAC* pamoja na ya TAMISEMI kwenye haya maeneo ambayo tunaelekeza fedha nyingi wakaweza kufanya ufuatiliaji sambamba na taasisi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimetoa ufafanuzi huu naomba sasa, Bunge lako liridhie bajeti hii na nawaomba Wabunge wote na naamini Halima Mdee kwa mara ya kwanza utapiga kura ya ndiyo. Wote tuipigie bajeti hii kura ya ndio kwa sababu inakwenda kufanya mapinduzi. Wote na wenzako, hii ni bajeti yetu, tumeshiriki kuitengeneza na angalieni vitita tunavyoondoka navyo kwa ajili ya miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waheshimiwa wananchi nifafanue tu hilo sio kila Mbunge atabeba kwenye *pickup* hizo fedha, bali zitakwenda kwenye Halmashauri zetu Wabunge wenu wameziomba tu, ila wasije wakafika kule wakasema Waziri aliwaambia mtakuja na hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono katika kiwango ambacho hakijapata kutokea. *(Makofi/Kicheko/ Vigelegele)*

Ahsante sana, ahsante Waheshimiwa Wabunge. Kusema ukweli katika uzoefu wangu wa miaka mingi kama Mbunge, kweli kabisa kutoka moyoni mwangu, sijawahi kuona Serikali ikija na uhitimishaji wa bajeti wa aina hii ya leo. *(Makofi)*

Kwa kweli sisi kama Wabunge tunapaswa kabisa kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa mapendekezo haya yaliyokuja ya Serikali leo. Kwa sababu pamoja na bajeti ile tuliyopitisha kwa maamuzi haya ya kodi za aina mbalimbali ambazo tumefanya, Mheshimiwa Waziri ametuchambulia jinsi ambavyo nyongeza ya mabilioni ya fedha yanavyoenda katika maji, barabara, makazi, katika afya, mikopo ya wanafunzi elimu ya juu, masuala ya reli, bwawa la umeme yaani zile shida za wananchi ambazo Waheshimiwa Wabunge huwa tunahangaika nazo kabisa, kabisa, kabisa, ni haijapata kutokea. *(Makofi)*

Tunaipongeza sana Serikali, mno kwa mtazamo huu. Mimi naamini tukiendelea hivi katika hii miaka miwili, mitatu inayokuja hii, mwaka 2025 basi tena yaani ni kuchukua, kuweka, waaah, basi hakuna jambo lingine kabisa, kabisa. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kuhusu utaratibu ni kwamba huwa Mheshimiwa Waziri akihitimisha hoja yoyote, Waziri yeyote, Spika hutakiwa kulihoji Bunge ili litoe uamuzi wake wa kupitisha au kutokupitisha hoja iliyotolewa. Lakini leo tunataka tukidhi matakwa ya Kikatiba kama nilivyowaambia kabla, Ibara ya 90(2)(b) na uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutokupitisha bajeti ya Serikali, utafanywa kwa kupiga kura ya wazi, kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja, tofauti na bajeti zingine ambazo huwa tunafanya ambapo, huwa ninahoji mnasema ndiyo au hapana na inakuwa imepita. Kwa hii ya leo ni kura ya wazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Katibu natumaini ameshajiandaa ambapo naomba sasa *Sergeant-At-Arms* hebu tupigie kengele kila Mbunge arudi ndani, huku aliyepo huko nje tunaendelea na upigaji wa kura. Kila Mbunge anapaswa kuwepo humu ndani leo na yeyote asiyekuwepo, basi Spika awe na taarifa kamili na za uhakika za kwa nini hayupo, kwa sababu jambo hili ni la Kikatiba na ni la lazima, sio hiari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa tunaendelea na zoezi la kupiga kura ambapo namuomba Katibu sasa aendelee na utaratibu. Katibu.

**KUPIGA KURA**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

Mhe. Dkt. Tulia Ackson……………………………………….Ndiyo
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa…………………………….Ndiyo
Mhe. Mussa Azzan Zungu…………………………………….Ndiyo
Mhe. Najma Murtaza Giga……………………………………Ndiyo
Mhe. David Mwakiposa Kihenzile……………………..……Ndiyo
Mhe. Prof. Adelardus Lubango Kilangi……………………..Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi…………………………Ndiyo
Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika…………………..Ndiyo
Mhe. Jenista Joachim Mhagama…………………………Ndiyo
Mhe. Anatropia Rwehikila Theonest……………………...Abstain
Mhe. Ummy Ally Mwalimu…………………..........…………...Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako……………………….Ndiyo

Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi…………………Ndiyo
Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani……………………Ndiyo
Mhe. Selemani Saidi Jafo…………………………………...Ndiyo
Mhe. Doto Mashaka Biteko………………………………Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene………………..Ndiyo
Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba……………………Ndiyo
Mhe. Innocent Lugha Bashungwa………………………..Ndiyo
Mhe. Mohamed Omar Mchengerwa……………………Ndiyo
Mhe. Elias John Kwandikwa………………..………………Ndiyo
Mhe. Jumaa Hamidu Aweso………………………………Ndiyo
Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro………………………Ndiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndungulile………………..Ndiyo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki…………………………Ndiyo
Mhe. Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima…………………Ndiyo
Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda…………………………Ndiyo
Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe……………………Ndiyo
Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho…………Ndiyo
Mhe. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula……………...Ndiyo
Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo……………………...Ndiyo
Mhe. Angeline Sylvester Mabula…………......……………Ndiyo
Mhe. Wiliam Tate Olenasha…………………........………Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni…………………………Ndiyo
Mhe. Hussein Mohamed Bashe……………………………Ndiyo
Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara…………………………..Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega……………………...…………Ndiyo
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel…………………………Ndiyo
